epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Oktoba 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581838
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# KUMEKUCHA

• **Tume** ya Rais ya Maboresho Kodi yaanza kupokea maoni... *Endelea ukurasa wa 2*

UKURASA WA 2

**AJALI MABASI ZAUA WATU 13, KUJERUHI 59**

UKURASA WA 3


**TCRA YATAKA UMAKINI KATIKA MATUMIZI YA AKILI MNEMBA**



UKURASA WA 3

**AFYA, ELIMU MIUNDOMBINU VYAMNG'ARISHA MWINYI MIAKA 4 MADARAKANI**






UKURASA WA 21

**ARTETA ATOA ONYO WACHEZAJI ARSENAL**

MIKEL Arteta amewaonya wachezaji Arsenal kwamba hawawezi kuendelea na kiwango chao cha utovu wa...




Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Ombeni Sefue, akizungumza na waandishi wa habari Ikulu jijini Dar es Salaam jana wakati akitoa taarifa kwa wananchi kuanza kazi kwa tume hiyo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

**RIPOTI YA UCHUNGUZI-3 WAKOPESHAJI MTANDAONI**

## Polisi yakiri vilio ni vingi, TCRA yadai 'haituhusu'

UKURASA 4



## Mwanadada aeleza chungu, tamu za safari ukombozi mwanamke wa Kimaasai

UKURASA 11

**MICHEZO** **DIARRA ATOA SIRI KUMZUIA ATEBA** UK.24

**KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Tume ya Rais ya Maboresho Kodi yaanza kupokea maoni

**Na Romana Mallya**

TUME ya Rais ya Maboresho ya Kodi imetangaza kuanza kukusanya maoni ya wadau, wakiwamo Watanzania wanaoishi nje ya nchi (diaspora).

Mifumo iliyoandaliwa kwa ajili ya kupokea maoni hayo ni pamoja na kiunganishi cha edodoso.gov.go.tz kwa kutumia namba ya dodoso 54497, barua pepe tume@taxretorm.go.tz na maboresho.kodi@taxreform.go.tz au kwa kutuma ujumbe mfupi kupitia simu za mkononi za 0748 755 677 na 0738 588 813.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue alisema jana Ikulu, Dar es Salaam wakati akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari kuwa: "Tunapenda kuwajulisha wananchi kuwa tume imeanza kazi na sasa iko tayari kushirikiana na kumsikiliza kila mdau, iwe mmoja mmoja au kupitia vyama vya kitaaluma, jumuiya za biashara na makundi mengine.

"Tume imeandaa namna bora ya kuratibu ushiriki wa wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji, taasisi za umma na binafsi, asasi za kiraia, wadau wa maendeleo, diaspora na wadau wote ili kutoa maoni na mapendekezo."

Balozi Sefue alisema watafanya mikutano na wananchi katika maeneo mbalimbali na kukutana na wawakilishi wa makundi. Alitoa wito kwa taasisi za elimu ya juu, utafiti na nyingine zinazoweza kuandaa mijadala kuhusu hayo wawasiliane na tume.

Pia alitoa wito kwa vyombo vya habari kuandaa majukwaa ya majadiliano kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi kisha kuandaa taarifa ambazo zitasaidia tume katika utekelezaji wa jukumu hilo.

Balozi Sefue alitoa wito kwa wananchi kutumia fursa hiyo adhimu kutoa maoni kuhusu changamoto na mapendekezo ya maboresho ya mifumo ya kodi na ukusanyaji wa mapato.

Alisema lengo ni mapendekezo yatakayowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan yaakisi uzoefu na maoni ya kila mwenye mchango wa kutoa katika kuboresha mfumo katika nchi.

Alisema tume hiyo imeundwa kutokana na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji kuhusu kero zinazotokana na mfumo wa kodi nchini.

"Kodi ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Rais Samia ameonesha utashi wa kisiasa wa kushughulikia changamoto hizo na hatua ya kwanza ni kufanya tathmini ya kina ya mfumo ulioko ili kuwa na msingi wa kufanya maboresho ambayo ni wazi yanahitajika," alisema.

Balozi Sefue alisema tume itasaidia kufanya tathmini hiyo kwa kushirikiana na wananchi wengi iwezekanavyo ili kuainisha changamoto zilizoko hasa umuhimu zaidi ni kukusanya mapendekezo yanayotekelezeka na yatakayosaidia kuongeza mapato ya serikali kwa njia iliyo rafiki na rahisi zaidi.

Balozi Sefue alisema katika kipindi cha miama mitatu iliyopita, pato halisi la taifa limekua kwa wastani wa asilimia 4.7, huku mapato ya kodi yakifikia wastani wa asilimia 12.1 ya pato la taifa.

"Kwa kawaida tungetarajia kasi ya ukuaji huu wa uchumi iendane sambamba na kasi ya ongezeko la mapato ya serikali.

"Lakini hali si hivyo, kiwango tulichokifikia cha asilimia 12.1 ya pato la taifa ni chini ya asilimia 15 ya pato la taifa inayohitajika katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ili kujenga uwezo wa kufikia malengo ya kimataifa ya maendeleo endelevu," alisema.

Alisema serikali imedhamiria kufikia kiwango hicho cha asilimia 15 ya pato la taifa ifikapo mwaka 2026/27 akitaka kuwa ni hatua itakayoongoza uwezo wa nchi kugharamia miradi ya maendeleo na kupunguza kiwango cha utegemezi wa mikopo na misaada.

Oktoba 4 mwaka huu, Rais Samia alizindua rasmi Tume ya Kutathmini na Kushauri kuhusu Maboresho ya Kodi nchini. Tume itakusanya maoni kwa miezi miwili au mitatu.


CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

**Tanzania Teachers' Union – TTU**

**INVITATION FOR TENDERS**

**Tender No. TTU/T/G/01/2024/2025**
**for**
**Supply of T-shirts and Caps**

**Invitation for Tenders**

**Date: October 23, 2024**

1. This Invitation for Tenders follows Tanzania Teachers' Union, which appeared in Tanzania Teachers' Union financial regulations 3rd Edition of 2018.
2. Tanzania Teachers' Union has set aside funds for the supply of T-shirts and Caps during the financial year 2024/2025.
3. Tanzania Teachers' Union now invites tenders from eligible Supplier to Supply T-shirts and Caps.
4. Tendering will be conducted through Competitive Tendering method specified in Tanzania Teachers' Union Financial Regulations 3rd edition of 2018.
5. Interested eligible Tenderers may obtain tender document physically at Tanzania Teachers' Union, and pay tender participation of non-refundable fee of Tanzania Shillings 500,000. Payment is performed through bank via account National Microfinance Bank (NMB) 20101300312 Name Tanzania Teachers' Union and collect set of Tendering Documents physically at Tanzania Teachers' Union Head quarter office, Jamhuri Stadium from 9:00 AM to 03:00 PM (Monday to Friday).
6. All Tenders must be physically submitted in the proper format, at or before 04/11/2024, 10:00AM. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend at TTU- Head quarter office, ground floor meeting room, Box 3077, Jamhuri Stadium Dodoma.

**General Secretary - TTU**
**Tanzania Teachers' Union – TTU**
**P.O.BOX 3077**
**DODOMA**


# Ajali mabasi zaua 13, kujeruhi 59

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU 13 wamefariki dunia na wengine 59 kujeruhiwa kutokana na ajali mbili za mabasi katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro.

Ajali hizo zimetokea siku nne baada ya ile ya Oktoba 19 mwaka huu katika eneo la Kikavu, Hai mkoani Kilimanjaro iliyohusisha magari matatu yakiwamo lori na Toyota Coaster na kuua watu 14 huku wengine 12 wakijeruhiwa.

Ajali ya kwanza ilihusisha mabasi mawili ya abiria kugongana katika eneo la Ukiliguru, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza ambayo ilisababisha vifo vya watu wanane na wengine 39 kujeruhiwa.

Mabasi hayo ni ya kampuni ya Nyehunge lenye namba za usajili T.281 EFG lililokuwa likitoka Morogoro kwenda Mwanza na Asante Rabi lenye namba za usajili T458 DYD lililokuwa likitoka Mwanza kwenda Arusha.

Ajali ya pili imehusisha gari aina ya Toyota Coaster, ikisababisha vifo vya waimbaji watano wa Kwaya ya Usharika wa Wazo Hill, Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na wengine 20 kujeruhiwa eneo la Kirinjiko, Same mkoani Kilimanjaro.

Magari yaliyohusisha ajali hiyo ni aina ya FAW lenye namba T 517 EAE na tela namba T 287 CYF ambalo liligonga kwa nyuma gari T 553 aina ya Toyota Hilux na kisha kupoteza mwelekeo na kwenda kugongana uso kwa uso na Toyota Coaster yenye namba T 525 DKP.

Katika ajali hiyo, watu sita walifariki dunia papo hapo na wengine wanane walifariki dunia njiani wakipelekwa hospitalini.

Akisimulia jana tukio hilo, mmoja wa manusura wa ajali hiyo, mwandishi wa habari Angelo Mwoleka, aliyekuwa akisafiri na Asante Rabi kwenda Arusha, alisema magari hayo yaligongana uso kwa uso na yeye kuumia kisha kupelekwa Hospitali ya Kamagana, Nyegezi, jijini Mwanza.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Dk. Clement Morabu, alithibitisha kupokea miili ya watu wakubwa saba na mtoto mmoja mwenye umri wa miezi tisa ambaye alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

Kuhusu majeruhi, Dk. Morabu alisema baada ya kupokea taarifa ya ajali hiyo, walifika moja kwa moja katika eneo la tukio na kukuta majeruhi wengine zaidi ya 50 na kufanya uchambuzi.

Alisema majeruhi 21 waliokuwa kwenye hali ya kawaida walipelekwa katika Kituo cha Afya Usagara.

"Wengine 18 tuliwapeleka katika hospitali ya wilaya na majeruhi wote 39 wanahudumiwa kwa usahihi na mpaka sasa kati yao, majeruhi wanne ambao walikuwa katika hali mbaya zaidi wakihitaji vipimo kama CT-Scan tumewapa rufani kwenda ika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando baada ya kuwa tumewapa huduma ya kwanza," alisema.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, DCP Wilbroad Mutafungwa, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi na dereva wa basi la Nyehunge na kuchepuka bila kuchukua tahadhari.

**WAIMBAJI WAFARIKI**

Waimbaji watano wa Kwaya ya Usharika wa Wazo Hill, Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wamepoteza maisha na wengine 20 kujeruhiwa katika ajali ya basi iliyotokea juzi alfajiri eneo la Kirinjiko, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro.

Wanakwaya waliopoteza maisha ajalini walikuwa wakitokea Dar es Salaam kwenda Machame, Wilaya ya Hai kushiriki maziko ya mwanakwaya mwenzao aliyefariki dunia siku tatu zilizopita wakati anajifungua.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni aliwataja waliofariki dunia na kutambuliwa ni Stephen Temba (40), Aurelia Swai (50), Neema Ngusi (35), Charles Mchome (63) na Maderina Mtenzi (58). Majeruhi ni Neema Mgolo (54), Happiness Msagati, Elinaike Mushi (48), Flora Kamnde (46), Joyce (66), Anold Uroki (49), Richard Lupatu na George Kilango (55).

Wengine ni Grace Macha (55), Herry Macha, Herry Macha (53), Haika Urio (51), Daniel Kilonzi (40), Evaline Muro (54), Martha (42), Easter Lukindo (56) na Habia Kasumuni (56).

## HABARI KITAIFA

# Wazazi-CCM wapongeza miaka minne ya Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar imeadhimisha miaka minne ya mafanikio ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwenye sekta ya afya, elimu, miundombinu ya barababra na utalii.

Akiongoza mjadala katika kongamano hilo lililohudhuriwa na wana-CCM pamoja na mawaziri wa SMZ lililofanyika visiwani hapa, Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Dk. Ayoub Rioba, alisema yapo mafanikio mengi yaliopatikana katika uongozi wake Dk. Mwinyi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa CCM, Dk. Stephen Wasira, akizungumzia utekelezaji wa Ilani ya CCM na umuhimu wa watu kujiandikisha kupiga kura, alisema miaka minne iliyopita, Dk. Hussein aliongoza bendera ya kuiongoza Zanzibar na mafanikio yaliyopatikana ni mengi ikiwamo kukua kwa uchumi na makusanyo ya mapato serikalini yameongezeka na kutia moyo.

Alisema ongezeko hilo limenufaisha jamii ya Zanzibar na kutoa mfano wa pensheni ya wazee imeongezeka kutoka Sh. 20,000 hadi 50,000 na uchumi ukikua mafanikio yanakwenda kwa walengwa na bila ya kukua kwa uchumi serikali haiwezi kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema pia bajeti ya kusaidia wazee wasiojiweza imeongezeka, mambo hayo yanatekeleza mapinduzi yaliyokusudiwa kwa kusaidia wazee wasiojiweza na Rais wa Kwanza wa Zanzibar alijenga nyumba za kuwalea wazee.

Alisema uchumi wa Zanzibar unategemea zaidi sekta ya utalii ambao umeongezeka na kwa kipindi cha miaka minne uwekezaji katika sekta hiyo umeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 784,947,180 na kufikia bilioni 382 na idadi ya watalii imeongezeka.

Alisema Dk. Mwinyi amesimamia elimu na idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 280,000 hadi 510,000 na kujenga shule 62 na madarasa zaidi ya 2000 kwa muda wa miaka minne.

Aidha, amejenga hospitali 10 za wilaya kila wilaya ina hospitali pamoja na hospitali mbili za mkoa.

Kuhusu uandikishaji wa wapigakura, alisema CCM inalengo ya kushinda uchaguzi na kukamata dola na kwamba ni wajibu wa wanachama kujiandikisha na kupiga kura katika uchaguzi mkuu na bila ya kupiga kura ushindi hautoweza kupatikana.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Vuai Ali Vuai akizungumza mchango wa jumuiya za chama hicho, alisema bila ya amani na utulivu nchini hakuna chochote kinachoweza kufanyika, viongozi wa nchi, Dk. Mwinyi na Dk. Samia pamoja na jumuiya za CCM wamesimamia kikamilifu kuwapo amani na utulivu.

Akizungumzia sekta ya elimu, Waziri wa elimu na mafunzo ya amali Lela Muhammed Mussa, alisema Dk. Mwinyi ameboresha mazingira rafiki ya kujisomea katika ngazi zote na kuwekeza fedha za kutosha kuhakikisha mazingira hayo yanafikiwa.

Alisema mwaka 2021 bajeti ya maendeleo katika sekta ya elimu ilikuwa Sh. bilioni 83.2, lakini kwa mwaka 2024 bajeti ni Sh. bilioni 518, kujenga madarasa 2,783, amejenga majengo ya shule ya ghorofa 35 ambazo zina maabara na maktaba za kisasa na zimeunganishwa na mkonga wa intaneti na wanafunzi kusoma kidijitali.

Akizungumza katika kongamano hilo, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema katika chaguzi zilizopita asilimia kubwa ya waliojiandikisha katika daftari la wapigakura huwa hawaendi kupiga kura na kutaka chama kuhakikisha watu wote wanaenda kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 wakati utakapofika.

Alisema uchaguzi ni kura hivyo ni vyema wananchi na wanachama kuhamasishwa kujiandikisha katika daftari la wapiga kura katika awamu ya pili katika daftari hilo na kila mwenye sifa kujiandikisha ili kuwa na sifa ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

Alisisitiza suala la amani na utulivu maana bila ya amani mafanikio yasingepatikana ambapo uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa kiwango kikubwa.

Aidha, katika miaka minne ya uongozi wake amevuka malengo ya ilani ya CCM kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Naye Makamu Pili wa Rais wa Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu, Hemed Suleiman Abdullah, alisema Rais Dk. Mwinyi ameleta maendeleo makubwa kwa wananchi ikiwamo afya, elimu, miundombinu ya barabara na sekta nyengine.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Mohammed Said Mohamed (Dimwa), alisema chama kinafarajika kuona Rais Mwinyi anafanya mambo mazuri kama aliyepewa dhamana ya uongozi katika kutekeleza ahadi kwa wananchi.

# TCRA yataka umakini matumizi akili mnemba

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imezitaka taasisi mbalimbali kuwa makini zinapochakata taarifa kwa kutumia akili mnemba (Artificial Inteligence - AI) ili kuepuka upotoshaji.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, aliyasema hayo jana katika mkutano uliojadili namna taasisi zinavyoweza kupata thamani kubwa wakati wa uchakataji wa taarifa walizonazo na kuboresha huduma zao.

Mkutano huo ulioandaliwa na Umoja wa Wakuu wa Kampuni na Taasisi (CEO Roundtable) uliwakutanisha pamoja wakuu wa taasisi binafsi na za serikali jijini Dar es Salaam.

Aliwakumbusha kuwa taarifa wanazoziweka kwenye Akili Mnemba ziwe zimekusanywa kwa misingi ya kisayansi ili ziwe sahihi, kinyume cha hapo wanaweza kutoa taarifa za kupotosha jamii kwa kuwa mfumo huo hauna uwezo wa kutambua kuwa taarifa hizo sio za kweli.

Dk. Jabir alisema licha ya AI kuwa na uwezo wa kuchakata taarifa na kufanya uamuzi kama binadamu, ili zifanye kazi ipasavyo ni lazima kuwe na taarifa nyingi zilizochakatwa ielekezwe ni aina gani ya taarifa inahitajika kutoka kwenye takwimu hizo.

Alisema AI inaweza kuchagiza ukuaji wa biashara kama ikitumiwa vizuri, akielekeza kuwa taarifa inapaswa ichakatwe vizuri ndipo iingizwe katika mfumo huo kwa ajili ya kusaidia kutafasiri kwa aina tofauti.

"Kwa hiyo Akili Mnemba inakuja huku mwisho kabisa kwamba umeshachakata takwimu zako zile, ndio unaweza kuitumia," alisema.

Alisema wameamua kuwa na vikao vya aina hiyo baada ya kugundua kuwa kuna taarifa nyingi zinakusanywa katika taasisi, hivyo ni muhimu kukutana pamoja kujadili namna wanavyoweza kuziongeza thamani na wazitumie kuboresha huduma zao.

"Wanaweza kupata aina ya bidhaa au huduma ambayo hapo awali walikuwa hawaipati au wakaboresha huduma zikawa bora zaidi kutokana na kuwa na uwezo wa kuzitafsiri takwimu au taarifa walizonazo," alisema.

Aidha, alisema mkutano huo ni muhimu kwa sababu kampuni hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa sana katika ukuaji wa uchumi wa kidigiti hivyo taarifa wanazozikusanya zina mchango mkubwa katika kuboresha biashara zao.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Soft Tech, Harish Bhatt, alisema takwimu zinasaidia kampuni kufanya uamuzi wa namna ya kuboresha biashara na kutoa huduma nzuri kwa wateja.

Alitolea mfano katika benki wanaweza kutumia takwimu kuamua aina gani ya mteja kumpa mkopo wa aina gani ili kupunguza hasara.

Mkuu wa Huduma, Masoko na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Norman Kiondo, alisema kama kampuni inahusika na ukusanyaji wa takwimu wamejifunza namna taarifa inavyoweza kusaidia wafanyabiashara kuboresha kazi zao.

Kwa maoni:
+255 677 020 701
Email:
customerrelations@guardian.co.tz

**TAARIFA YA KUTEULIWA KUWA MFILISI**

**AMMARA EVENTS LIMITED**

Taarifa inatolewa kuwa Wanachama wa kampuni iliyotajwa hapo juu yaani AMMARA EVENTS LIMITED yenye usajili namba 151674410 (kampuni) wameamua kufunga kampuni hii kwa hiari na kumteua Bw. Frank Ntabaye (Wakili) wa Jengo la Jewel, Ghorofa ya 2, Kiwanja Na. 493, Barabara ya Mwai Kibaki, Regent Estate, Mikocheni, Dar Es Salaam-Tanzania kuwa mfilisi kwa madhumuni ya kufunga kampuni, kuanzia tarehe 07 Augusti 2024.

Umma unaarifiwa ipasavyo.
Mtu yeyote mwenye madai dhidi ya kampuni anatakiwa ndani ya Siku Ishirini na Moja (21) baada ya kutolewa kwa taarifa hii, kumpelekea mfilisi maelezo kamili ya dai lake dhidi ya kampuni pamoja na vielelezo vinavyothibitisha madai hayo. Madai yasiyo na ushahidi wa kutosha yatatengwa na hayatashiriki kwenye mgao wowote utakaofanyika.

**Mawasiliano yote yapelekwe kwa:**

**Bw. Frank Ntabaye,**
**Jengo la Jewel, Ghorofa ya 2,**
**Kiwanja Na. 493 Dar Es Salaam – Tanzania**

**TAARIFA YA KUTEULIWA KUWA MFILISI**

**GALAXY AGRICULTURE AND FARMING CO. LIMITED**

Taarifa inatolewa kuwa Wanachama wa kampuni iliyotajwa hapo juu yaani GALAXY AGRICULTURE AND FARMING CO. LIMITED yenye usajili namba 153888450 (kampuni) wameamua kufunga kampuni hii kwa hiari na kumteua Bw. Frank Ntabaye (Wakili) wa Jengo la Jewel, Ghorofa ya 2, Kiwanja Na. 493, Barabara ya Mwai Kibaki, Regent Estate, Mikocheni, Dar Es Salaam-Tanzania kuwa mfilisi kwa madhumuni ya kufunga kampuni, kuanzia tarehe 01 Julai 2024.

Umma unaarifiwa ipasavyo.
Mtu yeyote mwenye madai dhidi ya kampuni anatakiwa ndani ya Siku Ishirini na Moja (21) baada ya kutolewa kwa taarifa hii, kumpelekea mfilisi maelezo kamili ya dai lake dhidi ya kampuni pamoja na vielelezo vinavyothibitisha madai hayo. Madai yasiyo na ushahidi wa kutosha yatatengwa na hayatashiriki kwenye mgao wowote utakaofanyika.

**Mawasiliano yote yapelekwe kwa:**

**Bw. Frank Ntabaye,**
**Jengo la Jewel, Ghorofa ya 2,**
**Kiwanja Na. 493 Dar Es Salaam – Tanzania**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
23.10.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya Ijumaa tarehe **25-10-2024 hadi tarehe 31-10-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Shinyanga** kupitia Dodoma, gari hiyo ina namba ya usajili: **T 133 CCP /T 877 EAU**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 19.00**
**Upana - mita 4.00**
**Kimo - mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Shinyanga** kupitia Dodoma, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

MIKOPO MTANDAONI

# Polisi yakiri vilio vingi, TCRA yadai 'haituhusu'

- Namba za kigeni zatumika; unapatiwa kidogo, unalipa maradufu; masharti yanaingilia faragha za mawasiliano...

Na Mwandishi Wetu

***Sehemu ya pili ya ripoti hii jana ilikuwa na ushuhuda wa wananchi walivyorejesha mikopo kwa riba kubwa na hata kudhalilishwa na wakopeshaji wa mtandaoni. Endelea na sehemu ya mwisho...***

UCHUNGUZI wa Nipashe umebaini baadhi ya namba za simu zinazotumika kudhalilisha wakopaji hazina utambulisho wa Tanzania, yaani ZIP CODE +255.

Katika ufuatiliaji wake, mwandishi alibaini kuwa kwa siku mtu mmoja anaweza kupigiwa simu na watu 10 tofauti wakizungumza jambo tofauti juu ya mkopo aliochukua.

Baadhi ya namba zinazotumika kuwapigia simu wakopaji ni pamoja na zenye utambulisho (ZIP CODE) +212; +231; +355; +265; +216; +237; +248; +508; +467; +269;+257; +417; +324; +923; +236 na +882.

Ilibainika pia wakati wa uchunguzi kuwa mkopaji anaweza kupigiwa kwa namba ileile mara nyingi, lakini namba ya utambulisho (ZIP CODE) inabadilika.

Mwandishi alirekodi jumla ya namba 25 baada ya watu wake wa karibu kukopa kuchukua mkopo mtandaoni.

Mmoja wa vijana walioajiriwa na moja ya taasisi inayotoa mikopo hiyo (jina lake tunahifadhi) alisema: "Sisi tumeajiriwa tunalipwa ujira kwa kadri ulivyoingiza. Inabidi umsumbue mtu hadi aone kero alipe fedha anayodaiwa.

"Unakuta alishalipa lakini tunaambiwa lazima alipe na nyongeza, tunawaundia makundi maana wakati wa kuchukua mkopo wanaridhia tuone mawasiliano yao yote."

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, DCP David Misime anathibitisha kuna malalamiko mengi yamefikishwa polisi kuhusiana na mikopo inayotolewa mtandaoni.

"Kuna malalamiko mengi sana. Mfano, kuna walioomba kukopa Sh. 500,000, wakapewa fedha pungufu, lakini wanapaswa kulipa mkopo wa Sh. 500,000 pamoja na riba.

"Wengine wamefikia mahali anapoingia mkataba anaambiwa tuma kiasi fulani kwanza. Mfano, anakopa Sh. 400,000 anaambiwa tuma Sh. 50,000 kwa ajili ya kugharamia mkopo, lakini baada ya muda ile application inapotea.

"Mtu anaposhindwa kurejesha mkopo, wakopeshaji wanasambaza ujumbe 'mkumbushe fulani anadaiwa vinginevyo hatua zitachukuliwa'," anasema.

Kamanda Misime anaonya kuwa huo ni unyanyasaji kwa kuwa wakati mtu anakopa hakumshirikisha anayetumiwa ujumbe; mkopeshaji anapotuma ujumbe wa aina hiyo ni kuvunja sheria.




DCP David Misime



Julai mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alitoa bungeni maelekezo kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kitendo cha Uhalifu wa Mtandaoni, kufuatilia na kuchunguza watu wanaotumia taarifa za waliowakopesha mtandaoni kudhalilisha.

Vilevile, Juni 4 mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Emmanuel Mkilia, alionya taasisi na watu binafsi wanaofanya vitendo vya udhalilishaji kwa kuchukua taarifa za wateja wao, akisisitiza kuwa ni kinyume cha sheria.

Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano wa Tume hiyo, Innocent Mungy, anasema wananchi wengi hawana uelewa wa kulinda taarifa binafsi.

"Aliyesajiliwa anajua kuna kanuni, ila wengi hawazifuati na tumebaini wanatumia taarifa za watu kuwadhalilisha au kupeleka taarifa binafsi kwa ndugu na marafiki. Hili ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022," anaonya.

Mungy anasema kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo, wakopeshaji wanatenda makosa mawili: Mosi, kuendesha shughuli zao mtandaoni pasi na kusajiliwa na pili, kutumia taarifa binafsi za watu na kuziweka mtandaoni kwa nia ya kuwadhalilisha na kuondoa haki ya faradha.

Anabainisha kuwa hadi sasa waliosajiliwa ni 580 na ambao wako kwenye mchakato ni 688. Malalamiko 28 yaliyopokewa, yako kwenye hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mjumbe wa Bodi ya Tume hiyo, Maxence Melo ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Forums, anasema zimeibuka App nyingi zinazotoa mikopo, lakini asilimia 90 wamemchukulia mwananchi kama fursa ya kunufaika na si mteja wa kuhudumiwa.

"Jamii Forums tumepokea malalamiko zaidi ya 800 taarifa zao kuibwa, makato makubwa, watu wanapata mkopo kwa dakika chache, ukishapata unageuka mtu anayejutia, wanasambaza picha zako, wanavunja haki ya faragha na Sheria ya Taarifa Binafsi, hii ni mbaya sana," anasema Melo.

Anashauri mamlaka zisiishie kukemea tu, bali wakamatwe na wananchi wawekewa utaratibu wa kidigitali ili watoe taarifa na ushahidi wa taarifa zote zilizochukuliwa, isiwe lazima kwenda Dodoma au ofisi za Tume ya Taarifa binafsi.

> **Kuna malalamiko mengi sana. Mfano, kuna walioomba kukopa Sh. 500,000, wakapewa fedha pungufu, lakini wanapaswa kulipa mkopo wa Sh. 500,000 pamoja na riba.**

Katika uchunguzi wake, mwandishi wa Nipashe alijisajili kwenye app ya CashX ambako alitakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa uraia (NIDA), picha, majina matatu, tarehe ya kuzaliwa, majina ya wadhamini wawili ambao lazima ataje uhusiano wake na watu hao, namba zao za simu na namba ya nyumba wanakoishi.

Mwandishi pia alitakiwa kutaja kiwango chake cha elimu, kazi anayofanya, hali ya ndoa yake, kipato chake kwa mwezi, siku ya malipo na barua pepe.

Pia walimtaka mwandishi atoe rukhsa rekodi ya simu yake kuhifadhiwa na wakopeshaji hao, wakiwa na maelezo: "Tutafuatilia tu ikiwa una rekodi za simu ili kuchanganua ikiwa unazitumia katika mazingira halisi ya kuzuia ulaghai. Tutahifadhi kwenye seva binafsi ya faragha na kuahidi kutoshiriki na mtu mwingine.

"Kuhusu eneo, tunafuatilia anwani ya IP pekee. Tutaihifadhi kwenye seva ya faragha na kuahidi kutoishiriki na mtu mwingine."

Kwenye kamera waliandika: "Tunahitaji kuthibitisha maelezo ya utambulisho wa mtumiaji na maelezo yanayohusiana ili kutusaidia kujua zaidi kuhusu watumiaji (KYC). Tutahifadhi kwenye seva binafsi na kuahidi kutoishirikisha na mtu mwingine."

Kuhusu kalenda ya mkopaji, waliandika: "Tunahitaji ufikiaji ili tuweze kukumbusha kufanya malipo kwa wakati katika kipindi cha kurejesha mkopo. Kipengele hiki kimeundwa ili kuboresha mchakato wa ulipaji na matumizi yako. Ikiwa hutawasha rukhsa hii, hutaweza kutumia sehemu mahususi inayohusiana na rukhsa hii."

Mwandishi alibaini kuwa mwombaji mkopo hawezi kuendelea na maombi yake ikiwa hatatoa rukhsa ya taarifa zake na anapokataa, huletewa ujumbe wa "Tafadhari tupe ufikiaji wa rukhsa yako ya simu kabla ya kutumia huduma zetu."

Agosti 19 mwaka huu, mwandishi aliwasilisha maswala TCRA akitaka kujua uhalali wa matumizi ya namba za simu zenye utambulisho (ZIP CODE) usio wa Tanzania zinazotumika kutoa mikopo na mtandaoni na kama app hizo zinatambuliwa na mamlaka hiyo.

Majibu yaliyotolewa na mamlaka hiyo ni haya: "TCRA inathibitisha kupokea maswali juu ya masuala ya mikopo mtandaoni. Tunapenda kutoa ufafanuzi kuwa masuala yote yanayohusu fedha, ikiwa ni pamoja na mikopo ya mitandaoni yanasimamiwa na BoT na masuala ya uhalifu mtandaoni yanashughulikiwa na Jeshi la Polisi Tanzania."

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Biashara mtandaoni zidhibitiwe, ni chanzo serikali kukosa mapato

**HIVI** karibuni kumeibuka wimbi la biashara na mikopo kwa njia ya mtandao. Kupitia mikopo na biashara hizo, baadhi ya kampuni hizo zinatumia mitandao ya kijamii na simu za mkononi kuhamasisha watu kununua bidhaa na kukopa fedha.

Katika uhamasishaji huo, kampuni zinazouza vifaa, vingi vikiwa vya nyumbani kama vile sufuria, vyombo vya umeme na kudai kuwa malipo ni baada ya bidhaa kumfikia mteja. Mteja anapouliza ofisi za kampuni hapewi majibu sahihi kwa kuwa hata anayefikisha mali ni wakala tu na si mmiliki wa duka au mfanyabiashara mwenye leseni ya kufanya hivyo.

Kwa kampuni zinazokopesha fedha, zimekuwa na vivutio vingi kama vile riba ndogo na inalipwa kwa miezi sita au zaidi. Kampuni moja kwa mfano, ijajinasibu kwamba inakopesha Sh. 600,000 hadi 900,000 na mteja atalipa kiwango kidogo cha fedha kwa siku hadi kwa mwezi. Kwa mujibu wa kampuni hiyo, mtu akikopa

Sh. 500,000 kwa mfano, atarejesha Sh. 50 kwa siku au 1,400 kwa mwezi.

Mikopo inayotolewa na kampuni hizo ambayo inatangazwa kwenye mitandao ya kijamii inatumika kama ulimbo kuwanasa baadhi ya Watanzania ambao wanachoangalia ni fedha na si kingine. Matokeo yake wanakuja kuyaona madhara baada ya kuwa wameshakopeshwa na kutambua kuwa ni kausha damu au mikopo umiza.

Aidha, kwa kampuni za uuzaji na usambazaji wa vyombo vya majumbani, nazo zimekuwa zikitumia mwanya huo kuwaumiza wateja kwa kuwa baadhi ya vifaa huwa vya kiwango duni na huharibika muda mfupi huku wakitoa waranti ya mwaka mmoja. Chombo kinapopata matatizo, hawashughuliki na mteja na wanamwambia kanuni yao ni kwamba chombo kikishauzwa hakirejeshwi. Licha ya kutoa kauli hizo, kampuni hizo ambazo pia baadhi zimekuwa zikipitisha vyombo majumbani, zimekuwa hazitoi risiti kuonyesha kuwa ni walipakodi halali.

Kutokana na kuwapo kwa biashara hizo na ukopeshaji wa kupitia mitandaoni, imebainika kwamba huo ni mwanya wa kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kwa kampuni zinazokopesha, zimebainika kuwa licha ya kutokulipa kodi halali, zinawatoza wananchi riba kubwa ambazo ni maumivu kwao.

Mmoja wa waathirika katika ripoti ya uchunguzi kuhusu mikopo hiyo iliyochapishwa jana na juzi kwenye gazeti hili, anasema alikopa Sh. 50,000 lakini alilipa Sh. 250,000. Hata alipogoma kulipa baada ya kubaini kuwa ni riba kubwa kuliko alivyoambiwa wakati akishawishiwa kukopa, alidhalilishwa kwa kuwekwa picha yake kwenye mtandao wa kijamii.

Katika kuonyesha mikopo hiyo kuwa imekithiri na inatweza na kudhalilisha utu wa mtu, Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA, Felista Njau, anasema katika utafiti wake alioufanya tangu mwaka 2020, amekutana na kero mbalimbali ikiwamo wakopeshaji kubadili majina ya taasisi hali inayoonesha kuna jambo lililojificha nyuma ya pazia.

Anasema katika utafiti huo, amebaini kuwa mtu anakopa Sh. 50,000 lakini analipa mpaka Sh. 175,000 na wanaokopa, asilimia 65 ni wanawake ambao wanaambiwa ni mikopo ya muda mfupi kuipata na haina usumbufu lakini baada ya kupata wanaanza kudaiwa na wale walio kwenye simu yake wanaarifiwa kuhusu jambo hilo.

Ni vyema sasa hatua zikachukuliwa na kukomesha mikopo hiyo ambayo inatweza utu wa mtu. Kwa kuwa wakopeshaji hao wanafahamika, sheria kali zichukuliwe dhidi yao. Maneno sasa yanatosha, vitendo zaidi vinatakiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Shirikisheni wananchi miradi ya maendeleo

**MWENGE** wa Uhuru umehitimisha mbio za mwaka 2024 Oktoba 14 jijini Mwanza, kinachofuata ni maandalizi ya ratiba nyingine mwakani.

Katika kilele cha mbio hizo wiki iliyopita, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, anasema miradi 16 yenye thamani ya Sh. bilioni 8.6 imekataliwa.

Anasema tayari miradi hiyo imekabidhiwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa hatua zaidi ili watakaohusika kuikwamisha, sheria ifuate mkondo wake.

Hatua hiyo ni nzuri na inaweza kusaidia kukomesha vitendo vya hujuma kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imekuwa ikihujumiwa kwa kutekelezwa chini ya kiwango.

Umefika wakati sasa ushirikishaji wananchi kulinda miundombinu ya miradi ya maendeleo upewe kipaumbele ili nao wawe na mchango utakaowezesha kuzuia hujuma.

Wananchi wakijua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao, gharama yake na jinsi inavyotekelezwa, inaweza kuwa rahisi kufuatilia kama kilichokusudiwa ndicho kinachotekelezwa.

Kama watabaini kuwa sicho, wanaweza kupaza sauti ili wahusika wachukuliwe hatua haraka, kuliko kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yao bila wao kujua kinachoendelea.

Yawezekana hawajui kuwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo ni ya serikali, hivyo hawahusiki kuifuatilia. Kama ndivyo wanavyodhani, basi waelimishwe ili wajue wajibu wao.

Inasikitisha kuona miradi ya mabilioni ya fedha ikikataliwa. Chanzo cha kutekelezwa chini ya kiwango ni ili sehemu ya fedha za mradi hiyo iingizwe kwenye mifuko na kuishia kwenye matumbo ya wachache.

Lakini kama wananchi wangejua kuwa miradi hiyo ni yao na wanatakiwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wake, pengine kusingekuwa na taarifa za kukataliwa, kwani yote ingetekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Hivyo, ingependekezwa kuwa kama wananchi watashirikishwa kikamilifu, hasa kwa kupewa elimu ya kujua muhimu wa kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ili nao waweze kuifuatilia, kukosoa na kuripotri upungufu.

Vinginevyo, hujuma katika miradi ya maendeleo inaweza kuendelea, kwani sidhani kama mwananchi anayejua umuhimu wa miradi ya maendeleo katika eneo lake anaweza kunyamazia hujuma.

Ikumbukwe kuwa, dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona wananchi wananufaika na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao, lakini inapokataliwa, ni kwamba ina kasoro.

Hujuma ni dhidi ya miradi ya maendeleo ni adui mkubwa ambaye anapaswa kupigwa vita na kila mpenda maendeleo, ili kodi za wananchi zitumike inavyotakiwa kwa ajili yao na taifa kwa ujumla.

Lakini pia ni vyema TAKUKURU nao wakawa wanafuatilia miradi hiyo tangu mwanzo ili iwe rahisi kubaini udanganyifu unaofanyika badala ya kusubiri kupelekewa taarifa ili wachunguze.

Kwa mtazamo wangu, kusubiri kupelekewa taarifa mezani ili waanze kuchunguza, kunawapa mwanya wajanja wachache kuendelea kufanya hujuma kwenye miradi na kujiimarisha kwa ajili ya kuficha ushahidi.

Maelekezo ambayo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amewahi kuyatoa kwa wakuu wa mikoa na wilaya, ni kwamba wasimamie miradi yote ya maendeleo kwenye maeneo yao na kuhakikisha inakamilishwa ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Katika maelekezo yake zaidi ni kwamba eneo la usimamizi wa miradi, wahakikishe wana taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo, wajiridhishe kama imekamilika au la, na kama bado haijakamilika, wafuatilie ili kujua ni kwa nini haijakamilika.

Ufuatiliaji unaweza kuja na majibu mazuri kwani unasaidia kujua kama kuna hujuma au uzembe. Lakini ushirikishwaji wa wananchi kudhibiti hujuma katika miradi ya maendeleo katika maeneo yao ni la muhimu.

HABARI KITAIFA

# Mkumbo avutiwa utendaji Bandari Dar

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo, amepongeza uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na kampuni ya kimataifa ya DP World katika Bandari ya Dar es Salaam.

Amesema serikali itaendelea kuboresho zaidi bandari hiyo katika maeneo mbalimbali ikiwamo makusanyo ya kodi kupitia Dira ya Taifa ya miaka 25 ijayo (2050).

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kikazi bandarini hapo na kusema uwekezaji uliofanyika ni mkubwa na una tija kwa taifa katika maeneo mbalimbali ikiwamo ukusanyaji wa mapato na ufanisi mkubwa katika utoaji wa huduma na kuvutia wafanyabiashara zaidi kutumia bandari hiyo.

"Nikiwa waziri mwenye dhamana katika sekta ya uwekezaji na mipango nimeamua kuitembelea Bandari ya Dar es Salaam ili kujionea utendaji wake kazi kupitia uwekezaji mkubwa uliofanyika," alisema.

"Kwa kweli nimefurahishwa sana na uboreshaji uliofanyika kimiundombinu na kiutendaji yaliyofanyika na haya ni matunda ya uwekezaji huu," alisema.

Aliipongeza menejimenti na uongozi wa (TPA) kwa usimamizi mzuri na mipango mbalimbali inayoendelea katika upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na nyingine ambayo itasaidia kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kupitia mipango ya Dira ya Taifa, Serikali inapenda kuona ni namna gani uwekezaji huo utazidi kuwa na tija katika miaka 25 ijayo kupitia mipango na mikakati mbalimbali ambayo serikali imeipanga.

Alisema uboreshaji unaoendelea kufanyika katika bandari hiyo kupitia uwekezaji uliofanyika utachochea uwekezaji katika sekta mbalimbali hapa nchini kama vile sekta ya viwanda mbalimbali, kilimo na elimu, ambazo zote zitasaidia kuleta tija kwa nchi ikiwamo kutoa ajira na kukuza uchumi.

"Namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu uwekezaji huu mkubwa na wa kihistoria kwa nchi yetu, kwa kuwa hivi sasa tumeanza kuona matunda yake," alisema Waziri Mkumbo.

Alibainisha namna uwekezaji huo utakavyoweza kukuza uchumi hasa katika mipango ya nchi ya muda mfupi na mipango ya muda mrefu na kuona kuwa yana tija kwa pande zote mbili, akimaanisha upande wa serikali na wa mwekezaji.

Kampuni ya kimataifa ya DP World imepewa kuwekeza kwenye gati namba nne mpaka saba na tangu ianze kazi imesaidia kuongezeka kwa mapato baada ya kuboresha miundombinu mbalimbali pamoja na kuweka gati na kupakua mizigo kwa muda mfupi tofauti na mwanzo.

# Sera ya Usafirishaji kufanyiwa marekebisho

**Na Christina Mwakangale**

SERA ya Taifa ya Usafirishaji ya mwaka 2003, inatarajiwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na mahitaji ya huduma za usafiri ardhini, kutokana na ujio wa safari za kisasa ardhini ikiwamo mabasi ya mwendokasi na treni ya SGR.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), Daud Daudi, aliyasema hayo jana, wakati baraza hilo likitia saini na Foundation for Civil Society (FCS), kwenye mradi wa kulinda, kutetea haki za watumiaji wa huduma za usafiri ardhini.

Akifafanua kuhusu mradi huo, Daudi alisema ni wa miaka mitatu hadi 2027 na unalenga kuboresha huduma za usafiri huo wa ardhini, baada ya kubaini kunahitajika elimu kwa umma kuhusu matumizi ya mifumo na miundombinu ya barabara.

"Mnafahamu kuna Sera ya Taifa ya Usafirishaji iliyoko Tanzania ni ya mwaka 2003. Kupitia Wizara ya Uchukuzi tupo katika mchakato wa kuiboresha, kwa sababu ikiboreshwa sisi tuna nafasi kubwa sana, kupenyeza maoni ya watumiaji.

Tangu mwaka 2003 ni miaka mingi na kwa wakati huo ukisema kutakuwa na usafiri wa SGR (treni ya kisasa) atakwambia ni ndoto za kusadikika, pia ukimwambia kutakuwa na usafiri wa mwendokasi kipindi hicho, angesema ataukuta akienda Ulaya. Ni jukumu letu, kupeleka maoni na yafanyiwe kazi," alisema Daudi.

Alisema baraza hilo hufanya kazi na wasafirishaji wa reli, waya na barabara, marejeo ya nauli hufanyika ili kuweka uwiano kulingana na thamani ya huduma kwa wakati husika na hali halisi ya maisha.

"Kwa miongo miwili, FCS wamejipambanua kufanya kazi na asasi na taasisi zisizo za umma, hata sisi mashirika ya kiserikali ni wadau wao. Wamekuja na mpango wa kuwafikia wananchi kuhusu huduma za usafiri ardhini ili kuja na kitu kinachoridhisha," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS), Justice Rutenge, alisema mradi huo na LATRA CCC umekuja, ili kuimarisha mifumo na huduma ya usafiri ardhini nchini na kufanikisha maendeleo ya nchi.


DTB DIAMOND TRUST BANK

**Diamond Trust Bank Tanzania kwenye Jukumu la Uwajibikaji kwa Jamii kupitia kampeni ya Namthamini**

Zanzibar, Oktoba 2024

Diamond Trust Bank Tanzania imejidhatiti kikamilifu kwenye kanuni endelevu na uwezeshaji wa maendeleo ya jamii. Mwaka huu kwa kushirikiana na East Africa Television, tumekamilisha kwa mafanikio kampeni ya Namthamini visiwani Zanzibar. Benki ilisambaza taulo za kike 315 zinazoweza kutumika tena, zinazojulikana kama Tumaini Kits kwa wasichana wa Shule ya Sekondari ya Mwera, Shule ya Sekondari ya Mwera Pongwe na Shule ya Msingi ya Moachi. Mpango huu ulilenga kushughulikia changamoto za afya ya hedhi zinazowakabili wasichana wadogo na kutoa rasilimali muhimu ya elimu yao inayoendelea.

Sambamba na usambazaji wa taulo za kike, mafunzo muhimu kuhusu afya ya hedhi, lishe bora na afya ya akili yalitolewa ili kuwawezesha wasichana kupata maarifa yatakayosaidia ukuaji wao binafsi na kitaaluma. Kampeni hii kwa kushirikiana na taasisi ya Zanzibar Maisha Bora (ZMBF) na East Africa Television itasaidia ama kupunguza suala la utoro unaosababishwa na ukosefu wa bidhaa za usafi wa hedhi pamoja na kuhakikisha wasichana hawa wadogo wanaweza kuzingatia elimu yao bila usumbufu.

Mpango huu unaangazia ari ya Diamond Trust Bank katika kuleta mabadiliko chanya kupitia mipango mbalimbali ya uwajibikaji kwa Jamii kwa kuzingatia uendelevu, uwezeshaji na ushirikishwaji wa kifedha huku ikichangia kikamilifu ustawi na mafanikio ya vijana hapa nchini.




*Wafanyakazi wa Diamond Trust Bank Tanzania wakitoa elimu ya fedha kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mwera, Shule ya Sekondari ya Mwera Pongwe na Shule ya Msingi ya Moachi ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii*




*Wafanyakazi wa Diamond Trust Bank Tanzania wakitoa elimu ya matumizi ya taulo za kike zinazoweza kutumika tena, zinazojulikana kama Tumaini Kits kwa wasichana wa Shule ya Sekondari ya Mwera, Shule ya Sekondari ya Mwera Pongwe na Shule ya Msingi ya Moachi.*

dtbtanzania

**Bank with us. Bank on us.**

**TANGAZO**

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

# UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-24 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,613 | 1,355 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,587 | 11,064 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,084 | 51,670 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,298 | 1,701 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,077 | 2,627 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 119,280 | 118,222 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,447 | 3,651 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,454 | 1,640 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **194,842** | **191,930** |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 28,087 | 29,731 |
| 18 | Amana za Wateja | 119,698 | 115,999 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 328 | 332 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 28 | 27 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,895 | 3,303 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 560 | 721 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **152,596** | **150,113** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **42,246** | **41,817** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 5,014 | 3,753 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 13,777 | 15,037 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,956 | 1,527 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,246** | **41,817** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 20,904 | 21,703 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,982 | 6,845 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,596 | 2,125 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 21.68% | 21.79% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.73% | 5.69% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82.47% | 82.58% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 61.22% | 61.60% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89.84% | 90.99% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.41% | -1.46% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.52% | -1.25% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 4,588 | 4,175 | 13,563 | 11,856 |
| 2 Gharama za Riba | 2,200 | 1,978 | 6,519 | 5,797 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **2,387** | **2,197** | **7,043** | **6,059** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (30) | (6) | (188) | (841) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 484 | 481 | 1,082 | 1,899 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **325** | **423** | **1,011** | **1,020** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 118 | 91 | 337 | 234 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 207 | 332 | 674 | 786 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,694** | **1,476** | **4,882** | **4,357** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 889 | 763 | 2,564 | 2,169 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 805 | 713 | 2,318 | 2,188 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **564** | **669** | **2,278** | **1,664** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 135 | 135 | 322 | 404 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **429** | **534** | **1,956** | **1,260** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka** | **429** | **534** | **1,956** | **1,260** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 34 | 34 | 34 | 34 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 80 | 99 | 121 | 78 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.16% | 1.39% | 1.58% | 1.19% |
| (ii) Wanahisa | 4.08% | 5.42% | 6.25% | 4.33% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 34.48% | 32.10% | 33.50% | 33.84% |
| (iv) Zinazozalisha | 5.41% | 5.26% | 5.37% | 5.00% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 564 | 698 | 2,278 | 1,664 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 672 | 729 | 1,641 | 2,413 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,532) | (6,289) | (10,654) | (4,800) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,055 | (2,159) | 1,398 | 11,288 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 6,145 | 8,879 | 13,055 | (3,814) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 428 | 119 | (137) | (645) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (776) | 204 | 3,106 | (466) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (135) | (94) | (322) | (404) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***7,421*** | ***2,088*** | ***10,366*** | ***5,236*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (19) | (19) | (7) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **-** | ***(19)*** | ***(19)*** | ***(7)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (989) | (989) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | ***(989)*** | ***(989)*** | **-** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **7,421** | **1,080** | **9,358** | **5,230** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 26,433 | 25,353 | 24,496 | 23,928 |
| | **Mwaka** | **33,854** | **26,433** | **33,854** | **29,158** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2024** | **21,500** | **-** | **16,564** | **3,753** | **-** | **-** | **41,817** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 429 | - | - | - | **429** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,260) | 1,260 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | - | | | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2024** | **21,500** | **-** | **15,732** | **5,014** | **-** | **-** | **42,246** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.01.2024** | **21,500** | **-** | **15,964** | **3,753** | **-** | **989** | **42,207** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 604 | - | - | - | **604** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | **(989)** | **(989)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (5) | - | - | - | **(5)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.03.2024** | **21,500** | **-** | **16,564** | **3,753** | **-** | **-** | **41,817** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31sepemba2024

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mr. Ashish Kumar Jha**<br>**Mkurugenzi Mkuu** | | **21.10.2024** |
| **Mr. Mahadhil M.Karwani**<br>**Mkuu wa Fedha** | | **21.10.2024** |
| **Mr. Allen Richard**<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | **21.10.2024** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi** | | **21.10.2024** |
| **2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi** | | **21.10.2024** |

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MOMBI YA KUONESHA NIA: UTOAJI HUDUMA WA SHUGHULI ZA USALAMA BAHARINI KUMBUKUMBU NA. REQ-00000639

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma za shughuli za usalama Baharini kwa ajili ya Mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) inahitaji huduma ya uhakika kwa ajili ya kusaidia shughuli za usalama baharini kwenye gati na vituo vya kupakulia mafuta (LOF) vilivyoko Chongoleani Tanga Tanzania wakati wa awamu ya utekelezaji wa maradi. Huduma hii itajumuisha Nyanja zifuatazo:

- Wafanyakazi: Utoaji wa wafanyakazi wenye ujuzi wa kusimamia na kuendesha masuala yote ya shughuli za usalama wa baharini. Hii ni pamoja na maafisa wa usalama, waendesha boti, mafundi kwa ajili ya matengenezo ya boti, na wafanyakazi wa usaidizi.
- Boti: Ugavi wa boti zinavyofaa zilizo na vifaa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli katika maji ya kina kirefu na kina kifupi. Boti hizi lazima ziwe na uwezo wa kufanya kazi mbalimbali za usalama, ikiwa ni pamoja na doria, ufuatiliaji, na kuitikia matukio kwa haraka.
- Kituo cha Usaidizi cha Ulinzi: Uanzishaji wa kituo cha Usaidizi cha Ulinzi chenye zana na vifaa kamili kitakachotumika kama kitovu cha uendeshaji wa shughuli za ulinzi. Kituo hiki kinapaswa kujumuisha miundombinu ya usimamizi, uratibu, na msaada wa usafirshaji na uendeshaji.
- Miundombinu na zana kwa ajili ya Matengenezo na huduma: Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa boti na zana zingine wa mara kwa mara. Hii inahakikisha kwamba zana zote zinawekwa katika hali ya bora na tayari kwa kutumika wakati wote.
- Miundombinu ya kuwezesha shughuli za Uzinduzi na Matengenezo ya boti: Uanzishwaji wa mifumo na miundombinu itakayowezesha ufanisi wa uzinduzi na ukarabati wa boti. Hii ni pamoja na ujenzi wa zege/hanamu kwa ajili ya uingizaji na utoaji wa boti baharini, winchi na vifaa vingine muhimu ili kuhakikisha uendeshaji mzuri.
- Uendeshaji wa shughuli kwa masaa 24 siku saba za wiki (24/7): Huduma lazima iwezeshe shughuli za usalama wa baharini kwa masaa 24 siku zote saba za wiki. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba wafanyakazi na vifaa vyote vinapatikana na vinafanya kazi wakati wote ili kukabiliana na matukio yoyote ya usalama.

**Mazingira ya Uendeshaji wa shughuli**

Mkataba utashughulikia uendeshaji wa shughuli katika maji ya kina kirefu na kina kifupi ndani ya maji ya pwani ya Ikweta nje ya Afrika Mashariki. Huduma lazima ikabiliane na changamoto za kipekee zinazosababishwa na mazingira haya, ikijumuisha mabadiliko ya kina cha maji, hali ya hewa na matishio ya usalama yanayoweza kutokea.

**VIGEZO VINGINE**

The provider must have a proven capability in providing maritime training, (practical and theory), for local national personnel. Mtoa huduma anapaswa kuwa na uwezo unaothibitika wa kutoa mafunzo ya maswala ya baharini, (kwa vitendo na nadharia) kwa wafanyakazi wa ndani wa kitaifa.

**VIGEZO MUHIMU VYA HUDUMA:**

**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Maelezo yanayoonesha uzoefu wa kufanya shughuli kama hizo kwa ufanisi katika kuunga mkono sekta ya O&G katika mazingira yasiyotabirika na yenye changamoto ya usalama wa baharini.
- Cheti cha usajili to BRELA na leseni ya Biashara (Ambatanisha nakala)
- Leseni ya Biashara.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Nakala ya ripoti rasmi ya Kampuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)
- Wasifu wa watendaji wakuu watakaohusika katika utoaji wa Huduma ikiwa ni pamoja na vyeti vyao, kiwango cha uhitimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika katika miradi mikuu ya mafuta na gesi.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Sera YA Haki za Binandamu.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa kuzingatia mafunzo ya VPSHR.
- Kampuni zinatarajiwa kutoa uthibitisho kwamba zina vyeti/vibali vyote vifuatavyo:
  - ISO 28000 (Inahitajika )
  - ISO 9001:2015 (inahitaajika)
  - ISO 14001 (inahitajika )
  - ISO 28007 (inahitajika )
  - ISO 45001:2018 (inahitajika)
  - ICOCA

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **22nd November 2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-000006396 – Utoaji huduma za shughuli za usalama Baharini kwa ajili ya Mradi wa EACOP**. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.**

**Kumbuka:** Mradi wa EACOP utakagua na kutathmini hati zinazotumwa na kampuni zinazoonesha ili kupata orodha ya kampuni zilizokidhi vigezo vya awali. Kampuni zilizofuzu pekee ndizo zitapokea mwaliko, kwa makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA), mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuendeleza wa mchakato wa zabuni.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA YA KUKODISHA MALORI YA MATENGENEZO YA MAGARI/GARAJI INAYOTEMEBEA NA MAGARI KWA AJILI UENDESHAJI WA SHUGHULI KATIKA ENEO LA MRADI NCHINI TANZANIA. KUMBUKUMBU NAMBA 0000000631

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma Malori ya matengenzo/Garaji inayotemebea Pamoja na magari kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli katika maeneo ya kazi .

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Ikiwa ni dhamira ya kampuni kuendeleza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa Raia wa Tanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, kampuni inahitaji kuduma kutoka kwenye makampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha ya usambazaji na utengenezaji wa malori yanayotoa huduma katika eneo la kazi kulingana na sifa, miongozo na maelekezo ya KAMPUNI na sheria na kanuni za Tanzania.

**Magari yafuatayo yanahitajika:**

- Lori / Gari matengezo au gereji inayotembea.
- Lori lenye kreni ya Hiab/ Lori lenye winchi ya kunyenyulia mizigo.
- Lori la HIAB/winchi yenye uwezo mkubwa.
- Lori la Msafa marefu lenye sehemu ya kulala.
- Magari ya uendeshaji wa shughuli aina ya pick -up.
- Mabasi ya abilia kwa ajili ya wafanyakazi.
- Bitumen / Chombo cha kutunzia Mafuta Ghafi.

**Huduma zitajumuisha:** Ukodishaji na usimamizi wa magari;Ukodishaji na usimamizi wa vipuri vya magari; Usimamizi kamili wa magari, ikijumuisha huduma zote za kila siku; Vifaa vya mawasiliano katika magari & kamera,vipuri na huduma; Huduma za usimamizi wa ajali, matengenezo na uokoaji; Huduma za matengenezo makubwa na madogo; Usaidizi wote wa madereva kupitia dawati maalum la usaidizi; Usimamizi kamili wa safari ndefu k.m., RFL, usafiri wa nje ya nchi, faini n.k.; Usimamizi wa haraka wa akaunti; Usimamizi Bora wa utoaji ripot za darasani na jukwaa la IT; Ushauri bora wa utendaji na huduma za ushauri; Mipango ya uboreshaji endelevu, ikijumuisha gharama sahihi za uendeshaji wa shuguli na utwaaji; Uhandisi wa magari ya masafa marefu ili kusimamia uchakavu wa magari, kwa kuzingatia zaidi sifa sitahiki za magari ya kibiashara, ulinganifu na uzingatiaji wa sheria; Msisitizo wa juu wa ubunifu na teknolojia ya upunguzaji wa kaboni.

KUMBUKA: Pamoja na hayo, mzabuni anatakiwa pia kutoa huduma za waendeshaji kwa kila lori na magari yaliyotolewa. Opereta au muendeshaji wa vifaa vya unyenyuzi wa mizigo anahitaji kuzingatia sheria au taratibu za unyenyuaji za EACOP.

**VIGEZO MUHIMU VYA HUDUMA:**

**Makampuni au mashirika yanayoonesha nia yanakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Cheti cha usajili chaBRELA cha hivi karibuni (ambatanisha nakala)
- Cheti cha Uthibitisho wa mamlaka husika ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) nk.
- Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa Leseni Halali ya Biashara.
- Uthibitisho wa uzoefu katika kutoa huduma sawa na hii katika miradi au makampuni husiani ikiwa ni pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa hivi karibuni.
- Wasifu wa wafanyakazi wakuu watakaoshiriki katika mradi ikiwa ni pamoja na viwango vya Elimu, uzoefu, na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Unashauriwa kuwasilisha Ushahidi wa usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa Sera za Kupambana na Rushwa, Kupambana na Rushwa, Uzingatiaji na Haki za Kibinadamu.

Makampuni ambayo yana nafasi, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma Maombi pamoja na nyaraka zilizoainishwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb)) maombi yatumwe kabla au saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), kabla au tarehe ya **10/11/2024**, kichwa cha barua pepe kitakuwa: **EOI-000000631 UTOAJI WA HUDUMA KUKODISHA MALORI YA MATENGEZZO YA MAGARI/GERAJI INAYOTEMEBEA NA MAGARRI KWA KWA AJILI UENEDSHAJI WA SHUGHULI KATIKA ENEO LA MRADI.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote ya kuonesha nia lazima ya andikwe kwa Kingereza.**

**Kumbuka:** Mradi wa EACOP utakagua na kutathmini hati zinazotumwa na kampuni zinazoonesha ili kupata orodha ya kampuni zilizokidhi vigezo vya awali. Kampuni zilizofuzu pekee ndizo zitapokea mwaliko, kwa makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA), mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuendeleza wa mchakato wa zabuni.



# Wizara yaombwa kujenga masoko ya ndizi mpakani

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwasa ameiomba Wizara ya Kilimo kujenga masoko ya kisasa ya kudumu ya ndizi maeneo ya mpakani ili kuongeza kipato kwa mkulima.

Mwassa alitoa ombi hilo baada ya kubaini kuwa chanzo cha zao hilo kuendelea kuuzwa kwa bei ndogo hususani mkoani Kagera huku likipatikana kwa gharama kubwa katika mikoa mingine na nchi jirani.

Akizungumza wakati wa kilele cha Maonesho ya Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo kwa mwaka huu kitaifa yamefanyika mkoani hapa, alisema licha ya Kagera kuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji ndizi nchini, bado mkulima anapata manufaa kidogo ikilinganishwa na wa mazao mengine.

Aliiomba wizara hiyo kujenga masoko hayo kwenye wilaya ambazo zinalima zao hilo kwa wingi ili kumnufaisha mkulima kwa kuuza kwa bei nzuri na taifa kupata mapato kwa kukusanya kodi.

Alisema masoko hayo yatawasaidia wakulima kupanua wigo wa masoko ya ndizi ya ndani na nje kwa wafanyabiashara kuwafuata shambani.

“Mkungu wa ndizi kilo 50 anaouza mkulima wa Bukoba, Karagwe, Kyerwa na Muleba ni Sh. 3,000 hadi 10,000 lakini kwenye mikoa mingine wanauza hadi Sh.40,000 hii sio sawa,” alisema Mwassa.

Akijibu ombi hilo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, David Silinde, aliahidi kulifanyia kazi.

Silinde, alisema takwimu zilizoko zinaonyesha kuwa hadi sasa Taifa linazalisha chakula kwa asilimia 128 sawa na ongezeko la chakula kila mwaka.

Alisema mwaka 2023/24 uzalishaji wa chakula nchini ulikuwa tani milioni 22.8 na mahitaji milioni 17.7 na kuwa na zaidi ya tani milioni 5.05.

Alisema serikali itahakikisha kilimo hicho cha ndizi kinatoka kuwa cha mazoea na kuwa cha uhakika kwa kuwawekea wakulima mategemeo ya umwagiliaji badala ya kusubiri msimu wa mvua.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk.Luzila John, akizungumza kwenye kikao maalumu na madaktari tarajali pamoja wafamasia juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Madaktari watakiwa kuepuka rushwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADAKTARI na wafamasia tarajali wametakiwa kujiepusha na vitendo kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wagonjwa, la sivyo watachukuliwa hatua.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Sinyanga, Dk. Luzila John, kwenye kikao maalumu na wataalamu hao.

Dk. John, aliwaambia wataalamu hao tarataji katika kikao hicho kilichofanyika hospitalini hapo kuwa serikali imekuwa ikiboresha huduma za afya ili wananchi wapate matibabu bora na kuokoa maisha yao.

“Kila mgonjwa ahudumiwe kwa haki na usawa, kuna wataalamu wanatoa huduma kwa kuangalia hadhi ya mtu, hiyo haitakiwi, mtibu mtu bila kumbagua kwa kufuata miongozo ya afya,” alisema.

Alisema rushwa ni adui mkubwa wa haki na ni kinyume na miongozo ya kazi.

Vilevile, aliwakumbusha kutumia lugha nzuri wanapowahudumia wagonjwa na kuwapatia mrejesho wa maendeleo ya hali zao kiafya ili kuwapata faraja.

Baadhi ya wataalamu hao, walisema kikao hicho kimewakumbusha kuzingatia majukumu yao kwa wakati kwa kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

**Kila mgonjwa ahudumiwe kwa haki na usawa, kuna wataalamu wanatoa huduma kwa kuangalia hadhi ya mtu, hiyo haitakiwi, mtibu mtu bila kumbagua kwa kufuata miongozo ya afya.**

# Wakulima wakacha kilimo cha mazoea watimkia cha kisasa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKULIMA zaidi ya 5,000 kutoka katika vyama vya ushirika zaidi ya 100 wamejiinua kiuchumi baada ya kuachana na kilimo cha mazoea kwa kufuata kilimo cha kisasa.

Wakulima hao ni wa kahawa na korosho kutoka mikoa ya Mtwara na Kilimanjaro, wameachana na kilimo na kujikita na kilimo hicho chini ya Uwezeshwaji na Ulimishaji kutoka Benki ya Ushirika Tanzania (CBT).

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi hundi ya Sh. milioni 10 kwa Umoja wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) wa Vyama vya Ushirika nchini (SCCULT) wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yanayoendelea mkoani Mwanza, Mwenyekiti wa Bodi ya Mpito ya CBT, Prof. Gervas Machimu, alisema lengo ni kuhakikisha wanainua vyama vya ushirika na wakulima nchini.

Machimu, alisema maadhimisho hayo ya siku nne yanatarajiwa kufungwa kesho na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Ushirika CBT, Yahya Kiyabo, alisema lengo kuwekeza katika ushirika ni kuhakikisha wanabadili kilimo kutoka cha mazoea na kuwa cha kisasa.

Kiyabo, alisema katika kipindi cha kuanzia 2020 hadi 2024, zaidi ya Sh. bilioni 10 zimewekezwa katika kilimo ili kuboresha upatikanaji wa pembejeo, ujenzi wa maghala pamoja na mashamba ya kisasa.

“Wakulima zaidi ya 5,000 kutoka katika vyama vya ushirika zaidi ya 100 vimewezeshwa kupitia mikopo pamoja na maboresho mbalimbali tangu zikiwa benki za ushirika za Tandahimba na Kilimanjaro ambazo zimeungana na kuipata CBT ambayo ilianza utendaji wake Oktoba 1, 2024,” alisema.

Mwenyekiti wa Umoja Vyama vya Akiba na Mikopo nchini (SCCULT), Aziza Mshana, alisema wanachama zaidi ya milioni 1.5 nchini.

Alisema wanachama hao ambao wamejiunga na vyama hivyo zaidi ya 961 wanaendelea na maboresho ya kilimo ili kufikia hatua ya kilimo cha kisasa na cha umwagiliaji.

“Katika kuhakikisha tunaongeza mitaji katika vyama vyetu tutaendelea kuvishauri pia vyama ambavyo havijajiunga kuhakikisha vyama hivyo ili kujengewa uwezo katika matumizi ya fedha na kuboresha shughuli za kilimo,” alisema Mshana.

Ukurasa 13




**WAFUGAJI WAMWAMBIA NCHIMBI**
**Licha ya kushinda kesi mahakamani hakuna anayewafidia 'walichoporwa'**

Ukurasa 14



**ELON MUSK**
**Ni bilionea anayelipa wapigakura Marekani**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 23, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


ROSE NJILO ANAPOELEZA

# Chungu, tamu safari ya kufikia mapinduzi ya ukombozi wa mwanamke wa Kimaasai

**Na Elizabeth Zaya**

MWAKA 1984 katika Kijiji cha Arash wilayani Ngorongoro mkoani Arusha, anazaliwa Rose Njilo, mwanamama shujaa mtetezi wa haki za wanawake katika jamii zinazodumisha mifumo kandamizi.

Ni mwasisi na mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya Mimutie Women Organization (WMO), iliyoundwa 2012 wilayani Ngorongoro, akilenga iwe sauti ya kutetea haki za wanawake na watoto wanaoishi kwenye jamii za pembezoni.

Rose, anataja mlolongo wa misukosuko ya ukatili wa kijinsia aliopitia, akigusia ndoa ya utotoni, alipoozwa na miaka 12, akiuita mwanzo wa machungu kwenye maisha yake. Jasiri huyo alijinasua licha ya kukutana na milima mirefu kufikia ukombozi, hakukata tamaa, aliendelea kupambana mpaka akajiokoa licha ya kwamba tayari alikuwa ameshapata watoto katika ndoa hiyo chungu.

Baada ya kujiokoa na ukatili, ukandamizaji, unyanyasaji na vipigo alivyokuwa akipitia aliona haitoshi, alitafuta njia nyingine ya kurudi tena kwenye jamii kuwanusuru wanawake wenzake waliokuwa wakipitia madhila kama yake.

Kabla ya kufika kwenye simulizi ya namna ya alivyojiokoa yeye na wengine, Rose anasimulia machungu aliyokutana nayo baada ya kuozeshwa katika umri huo wa miaka 12 na mwanaume asiyemfahamu, namna mila ya Kimaasai inavyomweka mwanamke kando, ikimwona asiye na msaada na laana katika jamii hiyo, asiyepewa nafasi katika jambo lolote liwe la nje au ndani ya jamii yake.




Rose Njilo mwanaharakati na mpigania haki za wanawake wa jamii ya Kimaasai. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

Katika simulizi yake kwa mwandishi wa Nipashe, anasema siku aliyoozeshwa ndio ilikuwa ya kwanza kukutanishwa na mwanaume huyo, na kwa sababu ya umri, aliamini kwamba huenda baada ya kutambulishwa angerejeshwa tena nyumbani kuishi na wazazi wake mpaka atakapofikia umri mkubwa zaidi.

## ALIVYOOZESHWA

"Nilikutana na changamoto ya kuozeshwa na miaka 12, nilikatishwa masomo nikiwa darasa la tano miongoni mwa wasichana wachache sana wa jamii yangu waliopata bahati ya kuandikishwa shule. Nilipelekwa kwa mume nikiwa sielewi chochote na sikujua napelekwa wapi, wala sikuwahi kukutanishwa na huyo mwanamume hapo kabla. Kwa utoto niliokuwa nao nilijua wakinipeleka wananirudisha tena nyumbani, tena mwanaume huyo nikimwangalia ni mzee."

"Nikawa naangalia mbona jua linazidi kukomaa na sirudishwi nyumbani, maana niliamini watanirudisha baadaye lakini ikafika mpaka usiku siku ikaisha. Siku ya pili kulikuwa na sherehe jirani na pale nilipopelekwa, nikawaona watu wa kwetu, nikatumia hiyo fursa kukimbia, lakini walinikimbiza wakanikamata na kunirudisha tena kwa huyo mwanaume."

Rose anasimulia kwamba baada ya hapo hakuwa na namna nyingine ya kutoroka kwa kuwa kila alipojaribu kutoroka alikosa msaada kwa jamii iliyomzunguka hata kwa ndugu zake wa karibu, hivyo aliendelea kuishi maisha yenye maumivu kila siku.

"Niliishi kama niko kuzimu na nikiwa nimetengwa kwa sababu sina pa kwenda, na jamii yote iliyonizunguka inakubaliana na hiyo hali, hata kama unaonekana uko kwenye hatari ya kufa haikusaidii, kwa hiyo nikaishi kwa miaka 10 na nikazaa watoto wanne, nikiishi maisha ya uchungu na sikuwahi kufurahi katika kipindi hicho chote. Niliteseka mno sababu mazingira niliyokuwa nayo nilikuwa mdogo kwa hiyo hata majukumu mengine yalikuwa yananishinda." Anasema.

Aidha, walipompeleka kwa mume hawakutambua kama ni mtoto, waliona ni mke, kwa hiyo ni mtu mzima hata aliposhindwa kufanya majukumu mengine aliyopewa walihesabu ni kiburi. Lakini wakati huo akawa anapitia ukatili wa aina nyingi ikiwamo vipigo, wakati mwingine mumewe kumvua nguo mbele ya watoto wake, kwa hiyo alipomwona anarudi nyumbani alikuwa anatetemeka.

Anasema, kuna kipindi akilala anaona kama kifo kinakuja, alikuwa anatoka nje na kukimbia, wakati mwingine akisikia jina lake limetajwa anashtuka na kwamba alifika wakati akikaa mahali, anakuwa haelewi kama jua limechomoza au limetua, akiathirika kisaikolojia kiasi kwamba hata akikutana na mtu analia, anakimbia asionane na watu na akienda mahali alitembea porini si barabarani ili asikutane na yeyote.

Kadhalika, anasema baada ya vipigo na manyanyaso kuzidi, mama jirani yake alimuonea huruma na akamuahidi kumpa nauli atoroke aende mbali.

"Alipoona mume wangu hayupo, aliniita, akanishauri niende mahakamani au kwa mwenyekiti wa kijiji nikamshtaki, lak-

INAENDELEA UK. 12

# Chungu, tamu safari ya kufikia mapinduzi ya ukombozi wa mwanamke wa Kimaasai

INATOKA UK. 11

ini sikukubali kwa sababu niliamini sitapata msaada, huenda itaongeza zaidi tatizo nikiamini wote ni wale wale wa jamii ya Kimasai, akanipa nauli nitoroke."

Anaongeza: "Lakini niliporudi nyumbani nikajifikiria, nikaenda kwa mwenyekiti wa kijiji, baada ya kumweleza kila kitu hakuamini na akaniambia natakiwa kuvumilia...nilienda mara nyingi mwishowe nikaona bora nitoroke, nikamfuata tena yule mama aliyesema atanipa nauli akanisaidia, nikaenda kuwaacha watoto kwa ndugu zangu nikaondoka."

**KUPATA TALAKA**

Rose anasema muda kidogo baada ya kutoroka, alipata taarifa kwamba mumewe amekuwa akiwafuata wanawe huko alikowaacha na kuwatesa, kwa hiyo ilibidi arudi kuwaokoa kwa kufuata taratibu za kisheria.

"Nililazimika kurudi tena nyumbani wakati huo hata kule nilikotorokea maisha yalikuwa bado ni magumu kwa sababu sikuwa na kazi ya kufanya, niliishi kwa rafiki yangu wa kike aliyekuwa ananisaidia, lakini nilirudi hivyo hivyo kudai watoto kwa mume wangu, nilikwenda mahakamani, nikaelezea mateso wanayopata, nikatendewa haki, tukatalikiana na nikapewa watoto wangu licha ya danadana nyingi kwa sababu alikuwa anatoa hongo sana," anasema Rose.

**KUANZISHA SHIRIKA**

Anasema licha ya kuachana na mume, mawazo ya kunyanyasika aliyokuwa anapitia yaliendelea kumtesa na wakati akiwa katika hali hiyo, alipata wazo la kuanzisha taasisi ambayo itakuwa sauti ya wanaopitia madhila kama yake, aliunda shirika licha ya kuwa hakuwa na kipato wala kipato cha kumsaidia.

"Kwa hiyo mwaka 2012 nikaanzisha taasisi yangu, lakini hata hivyo elimu pamoja na lugha ya Kiingereza ilikuwa kikwazo tena kwa maana kwa mara ya kwanza nilikutana na mfadhili wa kunisaidia alikuwa ni Mzungu na alikuwa hajui Kiswahili, hata nilipotumia wale watafsiri wa lugha niliona kama kuna vitu hawamwambii ukweli kwa hiyo nikapata changamoto ya kujifunza Kiingereza.

"Nikatoka hapo nikamtafuta mzee mmoja kumwelezea ninachotaka kukifanya, akanishangaa nitawezaje wakati sijasoma, lakini baadaye akanisaidia namna ya kuandika katiba na kusajili, na ikabidi nisome pia Kiingereza, nikasoma na kompyuta na ndipo nikaanza rasmi safari ya kupambania maisha ya wanawake wenzangu wanaopitia unyanyasaji na ukatili kama mimi, nikilenga zaidi jamii ya kimaasai. Anasimulia kwamba hata baada ya kuanzisha taasisi yake hiyo mwanzoni hali haikuwa nzuri na kwamba alitumia fedha hata aliyopewa na ndugu au rafiki yake kama ya kujikimu, akiitumia kwenda kusaidia watu wanaopitia ukatili.



Rose Njilo akizungumza na mwandishi Elizabeth Zaya. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**KULETA MAPINDUZI**

Rose nasema mara ya kwanza kupata ufadhili ilikuwa mwaka 2017 na ndio mwaka alianza kwenda Ngorongoro kutoa elimu ya kupambana na ukatili wanaofanyiwa mabinti na wanawake akiwaelimisha watambue umuhimu wa elimu pamoja na kumthamini mtoto wa kike na mwanamke kama alivyo mwanaume.

Anasema haikuwa rahisi kwa sababu wengi wanaamini haiwezekani mwanamke kama yeye hasa ambaye jamii inamfahamu kila kitu alichopitia, kubadilisha mila na tamaduni ambazo zimeheshimiwa miaka yote halafu atokee na kutaka kuzibadilisha kirahisi.

"Niliona nianzie kwenye jamii yangu kwa sababu wenyewe wanaamini na waliendelea kushikilia msimamo wao kwamba mtoto wa kike katika jamii ya kimasai hahesabiki kama binadamu wengine, ni laana na hahesabiwi haki yoyote, na ukizaliwa wa kike unahesabiwa kama wa kuuzwa, yaani ni wa kubadilishwa na kupata mali ikiwamo mifugo kwa familia.

"Kwa maana hiyo, mila hizo ziliendelea kuumiza watoto wa kike, kudidimiza haki zao lakini pia kuwaweka katika mazingira magumu na hatarishi kama ilivyotokea kwangu, ukatili wa mtoto wa kike ulikuwa ukianzia siku ya kwanza tu mama anapojifungua, kwa sababu kama kuna watoto wawili wamezaliwa, yule aliyejifungua wa kike hawezi kupewa huduma sawa na yule aliyejifungua wa kiume, kulikuwa na ubaguzi mkubwa. Kwa hiyo nilipopata fursa hiyo nikasema lazima nipambane kubadilisha hili, niokoe watoto wa kike katika jamii yangu wanaoendelea kuangamia.

"Na hata mtoto wa kike alikuwa akifanya kosa hata kwa bahati mbaya, anayeadhibiwa ni mama yake kwa sababu walikuwa wanaamini kwamba ni ujinga wa mama yake. Kwa hiyo sikukubali, niliingia mzima mzima kwa hasira kama simba aliyechokozwa bila kujali nitakutana na misukosuko gani, sikujihurumia kwa sababu tayari kama ni ukatili nilikuwa nimepitia vya kutosha mpaka nikafikia hatua ya kujikatia tamaa kwamba mimi ni wa kufa tu.

**KUZUILIWA KUTOA ELIMU**

Rose anasimulia kwamba walivyomwona amerudi tena kwenye jamii yake na kuanza kutoa elimu kuhusu kuachana na mila hizo kandamizi, alianza kuchukiwa hadi na viongozi wa serikali za vijiji wakimfukuza aondoke kwa kuwa elimu anayotoa inawapotosha wanawake kuzikana tamaduni zao ambazo zilianzishwa tangu vizazi.

"Kwa hiyo hali ilikuwa ni mbaya kila mtu alikuwa ananichukia, wakaanza na kunibatiza majina mabaya, mara ohh ni malaya, nimeachana na mume wangu, nimekengeuka mila na tamaduni za jamii yangu, kwa hiyo niondoke nisiwaharibu wanawake wengine...jamii yote ya kimaasai ikawa inaniona mimi ni mbaya na ni adui yao. Na wakati huo wazazi wangu walikuwa wamefariki, kwa hiyo sikuwa na mtu yeyote wa kunitetea.

Rose anasema ndugu zake wakiwamo dada zake walikuwa wanashindwa wafanye nini bdala yake walibaki kuumia na kuteseka kwa namna jamii inavyomuona na kumchukulia.

"Lakini kwa yale madhila niliyopitia yalinijengea ujasiri mkubwa sana ambao pamoja na vita kubwa niliyokuwa nikipitia kutoka jamii ile niliendelea kuwa na nguvu ya kupambana. Siku moja ilifikia hatua Mwenyekiti wa kijiji akanitolea sime eti anichome nayo kisa eti nawakusanya wanawake kuwapa elimu wasikubali kukandamizwa, lakini nashukuru walioniokoa siku ile walikuwa wanawake wenyewe, walisimama wote kuwa upande wangu wakanitetea, wakawa wanasema Rose ni Mmasai kama sisi, kwa hiyo hatuwezi kuona kila siku mnamnyanyasa, ikabidi wakawa upande wangu.

"Mwenyekiti wa kijiji akaogopa, maana walimwambia ukimgusa tena na sisi tunakugeukia wewe na tunakuja kukulaani, nilishangaa sana ujasiri ulioonesha na akina mama wale kwa mara ya kwanza kusimama na kumbishia mwanaume tena kiongozi wao, nikashukuru sana kwamba angalau elimu niliyokuwa nimeanza kuwapatia imewaingia, hapo ndipo nikaanza kupata watetezi kwa jamii ile," anasimulia Rose.

Rose anasema, baada ya siku ile, walewale wanawake waliomtetea ndio waligeuka wakaanza kuelimisha na wengine kwenye jamii ile namna ya kubadili mitizamo yao kuhusu mila kandamizi ambazo wameziamini kwa miaka mingi huku wao ndio wakiwa waathirika.

**NABII HAKUBALIKI KWAO**

Anasema pamoja na kwamba elimu ilikuwa imeanza kuenea lakini kuna watu walikuwa wanaendelea kupambana naye wakimwendea na kumshauri aachane na kazi yake hiyo, wakimwambia nabii hakubaliki kwao, hivyo asiendelee ili asije kupatwa na madhara na kwamba miongoni waliompa ushauri huo walikuwapo pia baadhi ya madiwani kutoka kwenye baadhi ya Kata za wilaya hiyo ya Ngorongoro.

Rose anasema aliwasikiliza lakini hakukata tamaa akaendelea na kazi yake hiyo ya kutoa elimu katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ya Ngorongoro, na kwamba wale waliokuwa wanamwelewa aliendelea nao na wale waliokataa aliwapa muda.

Anasema ilikuwa kama dhambi na laana kwa mwanamke wa kimasai kusimama kwenye kikao cha maendeleo ya kijiji au mkutano wa hadhara, kuzungumza hata kama kuna shida kubwa wanayotamani kusema kwenye mkutano wa viongozi wa serikali.

"Na hata ikilazimika ukitaka kusimama ni lazima uende ukatafute majani mabichi ushikilie mkononi ndio uruhusiwe kuzungumza na ile ukishika hayo ni ishara kwamba wewe ni dhaifu ambaye hustahili kwa sababu inaaminika kwamba mwanamke akisimama ni laana kwa hiyo unashika hayo majani ili ile laana iondoke. Unakuwa umesalenda na unaomba msamaha kwa sababu mwanamke hustahili kusimama.

Lakini hata hiyo kusimama ni lazima kuwe kuna kitu cha msingi sana ambacho kimetokea umeshindwa kuvumilia, kwa hiyo inakuwa kama umejitoa mhanga na kila mtu anakutolea jicho kwa sababu siyo hali ya kawaida kuona mwanamke amesimama kijasiri.

"Hata mkisafiri kwenye gari ukiwa mwanamke, wanakuona kama laana kwa hiyo wanaweka jiwe kwenye gari ili isipate ajali, maana bila hivyo wanaamini hiyo laana yako itasababisha ajali. Unaweza pata picha ni namna gani mila za kimasai mwanamke si baraka bali laana," anasimulia Rose.

***ITAENDELEA WIKI IJAYO***

### WAFUGAJI WAMWAMBIA NCHIMBI

# Licha ya kushinda kesi mahakamani hakuna anayewafidia 'walichoporwa'

**NA HALFANI CHUSI**




Katibu Mkuu wa CCM Dk. Emmanuel Nchimbi, akuhutubia mkoani Simiyu. **PICHA: HALFANI CHUSI**

ZIARA ya Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, mkoani Simiyu imeahidi kutoa mwanga kwa wafugaji waliodhulumiwa haki yao baada ya kushinda kesi mahakamani.

Ni wilayani Meatu, anapoarifiwa kuwa licha ya baadhi ya wafugaji kushinda kesi ya kutaifishiwa mifugo yao, miaka mitatu iliyopita hata leo hawajalipwa.

Mbali na kero za wananchi pia ziara hiyo, inajikita kuangalia uhai wa chama, kuhamasisha watu kujitokeza kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na pia mambo yanayokwamisha maendeleo kama kuwanyima wananchi haki zao.

Akipinga unyanyasaji, wilayani Meatu, Dk. Nchimbi, anasema hatavumilia mambo yanayofanywa kinyume cha sheria na viongozi serikalini, akisema ni muumini wa utawala wa sheria.

Ni baada ya Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, kudai kuwapo kwa wafugaji ambao mifugo yao ilitaifishwa na kushinda kesi mahakamani miaka mitatu iliyopita lakini mpaka leo hawajalipwa.

"Nitalibeba suala hilo mpaka nihakikishe haki inapatikana kama walishinda kesi mahakamani hatupaswi kuwakimbia," anaahidi Nchimbi.

Baada ya hoja za Mpina, Nchimbi anasema chama kitatetea wananchi wanyonge na kuwashirikisha katika masuala yote muhimu.

Akiwa Bariadi, Dk. Nchimbi aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, anapokea kero ya soko na stendi akisema serikali itazitatua.

Hata hivyo, pamoja na majibu hayo kwa wananchi, anawasiliana kwa simu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, kutoa ufafanuzi kwa wananchi waliokuwa na shauku ya kujua ufumbuzi wa changamoto hizo.

Akijibu Mchengerwa anasema: "Rais amezingatia malalamiko hayo na ametuelekeza eneo hilo linapelekewa fedha ya ujenzi wa soko na barabara.

"Tutakuwa hapo Lamadi kuanzia mwezi ujao kufanya maboresho kwa sababu fedha tulionayo inalenga kujenga soko la kisasa na barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilomita nane," anasema Mchengerwa kwa simu na kushangiliwa na Wanalamadi.

Anaongeza kuwa wataalamu watakaokwenda mategemeo yao ni kufanya tathmini na kuongeza ujenzi wa stendi na kwamba kuanzia mwezi ujao wanategemea kutangaza zabuni ya ujenzi wa soko la kisasa na barabara.

Akikata simu ya Mchengerwa katika mkutano huo, Dk. Nchimbi alirusha dongo kwa vyama vya upinzani kwamba havina mipango thabiti ya kuongoza nchi.

"Kiongozi madhubuti anazungumzia mipango ya kuongoza nchi. Lakini vyama vya upinzani wakipata nafasi wanazungumza maandamano, kuchana kanga na kuzomea.

"Viongozi wa CCM wanaandaliwa, hakuna kiongozi ndani ya chama atakaa miaka 40. CCM itaendelea kuwa chama kijana zaidi kwani ina viongozi vijana na wazee wenye kuwalea vyema," anasisitiza.

Anatoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na CCM akisisitiza chama hicho kina nia njema ya kuwatumikia wananchi.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika mwezi huu anatoa rai kwa wananchi kujitokeza kwa wingi akiahidi kuwa chama chake kitateua wagombea wenye kujali changamoto za wananchi na siyo maslahi binafsi.

Akiwa Lamadi anaahidi chama hicho kitatoa 2,000,000 kuunga mkono ujenzi wa vituo vya madereva wa bodaboda katika mji wanaolalamikia kuteseka na jua.

**UMOJA, AMANI**

Kwa wakazi wa Bariadi, kiongozi huyo anasisitiza umoja, amani na mshikamano na kwamba hiyo ndio njia ya kuliunganisha taifa.

Anasema ndicho kitu cha thamani taifa lilichonacho kuliko kingine chochote, na hivyo, Watanzania lazima walinde kwa wivu mkubwa.

"Watanzania wa vyama vyote tunapaswa tujue jambo ambalo tulilonalo lenye thamani kubwa ni amani, umoja, mshikamano wa taifa letu," anasema Nchimbi.

> "Tunapenda na tunataka kuwa na Rais ambaye anaweza kuonyesha kwa vitendo kwamba anapenda watu wake, kwa jinsi anavyohangaika kutafuta fedha za miradi ya maendeleo lakini anavyoisimamia na kuhakikisha inatekelezwa."

Anasema kila anayejaribu kuvuruga umoja aambiwe kwamba hatupo tayari kuvumilia nchi iingie katika machafuko.

Anamsifu Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuonyesha kwa vitendo kuwa anawapenda watu wake kwa kuhangaika kutafuta fedha za miradi ya maendeleo, kusimamia na kuhakikisha inatekelezwa.

"Tunapenda na tunataka kuwa na Rais ambaye anaweza kuonyesha kwa vitendo kwamba anapenda watu wake, kwa jinsi anavyohangaika kutafuta fedha za miradi ya maendeleo lakini anavyoisimamia na kuhakikisha inatekelezwa."

"Kwa hiyo kazi tuliyonayo ni ya kuendelea kumuunga mkono ili aendelee kuitumikia nchi yetu kwa uaminifu, upendo mkubwa na nchi yetu iendelee kupata maendeleo." Anasisitiza Nchimbi.

**MAKALLA**

Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, anapozungumzia uchaguzi anasema kuhamasisha wananchi kujiandikisha, kuweka mawakala waaminifu kisha kuhimiza kujitokeza kwa wingi katika upigaji kura.

Anaahidi chama kitateua wagombea wenye sifa ya kuwatumikia wananchi, akidai upinzani umepoteza sera, unazungumzia udini, ukabila, kuchoma moto kanga, lakini ruzuku wanazopata hawachomi.

"Rais Dk. Samia amerejesha mikutano ya kisiasa, akawarudishia ruzuku waliyokuwa wanadai, lakini ruzuku hawarudishi. Tunawaeleza kwamba CCM itashinda kwa haki kwani inaungwa mkono na Watanzania," anasisitiza.

**HAKUNA MAENDELEO**

Kada wa CCM aliyejiengua CHADEMA, Peter Msigwa anasema Tanzania iko salama chini ya uongozi wa chama hicho na kwamba wanaodhani vyama vya upinzani vitawaletea maendeleo wafumbue macho kwani vimebaki kile anachokiita kulialia.

Anasema alikuwapo huko kwa zaidi ya miaka 20, ameona hakuna maendeleo wala demokrasia, akisisitiza kwamba Rais Samia ameua upinzani kwa vitendo.

"Niwaombe wananchi tujitokeze kuchagua viongozi wanaotokana na chama hiki wala msidanganyike kule hakuna viongozi wa kuendesha nchi

"Ninaomba niwaulize kati ya sungura na mamba nani anayajua maji vizuri? Mimi ni kama mamba kwa CHADEMA naijua ndani na nje," anasema Msigwa.

Katibu wa NEC Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, anawataka vijana kujituma na kufanya kazi za kuwaingizia kipato akiwahimiza kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia 10 inayotarajiwa kuanza kutolewa muda wowote kuanzia sasa.

Mikopo hiyo ya halmashauri hutolewa kwa wanawake asilimia nne, vijana kiwango hicho na wenye mahitaji maalumu hupata asilimia mbili, ikipewa jina la uwiano wa 4:4:2.

ELON MUSK

# Ni bilionea anayelipa wapigakura Marekani

## •Mfuasi kindakindaki wa Donald Trump



Elon Musk akizungumza jijini Pennsylvania. **PICHA: REUTERS**

**Na Mwandishi Wetu**

BILIONEA namba moja duniani Elon Musk, anamwaga dola kama njugu kwa wanaojiandikisha kupiga kura, akitoa Dola 1,000,000 kila siku kwa anayeshinda kupitia bahati nasibu.

Maswali yanaibuka kuhusu uhalali wa pesa za bilionea huyo wa teknolojia kwa wapigakura wa majimbo mbalimbali wanaotia saini ombi lake la America PAC, kabla ya uchaguzi wa Marekani unaofanyika Jumanne Novemba 5, 2024.

Ni ombi la kampeni la Musk la America PAC, lilianzishwa kuunga mkono Donald Trump katika kinyang'anyiro cha urais.

Lakini, wataalamu wa sheria wanasema huenda hilo linavunja sheria ya Marekani kutoa pesa kwa mtu aliyesajiliwa kama mpigakura.

PAC inawahimiza wapigakura wa majimbo ya Georgia, Nevada, Arizona, Michigan, Wisconsin na North Carolina kusaini kuunga mkono uhuru wa kujieleza na haki ya kubeba silaha.

Aidha, wale wanaoleta mpigakura atakayesaini hupokea Dola milioni 47. Kiasi cha juu ni dola milioni 100 kwa kusaini au kumleta mtu wa kusaini hutolewa huko Pennsylvania, jimbo ambalo ni uwanja wa vita kati ya Trump na Harris na kura zao huko zinaaminiwa zinaweza kuamua mshindi wa mwisho.

Amerika PAC inasema wale wanaotia saini ombi hilo wanaashiria kuunga mkono kifungu cha kwanza na cha pili cha katiba ya Marekani.

Kila siku hadi Novemba 5, zawadi ya dola milioni 1 itatolewa katika mfumo wa bahati nasibu kwa yeyote aliyetia saini mojawapo ya majimbo saba.

"Naamini pesa ya Musk inaweza kuwa ni kinyume cha sheria," anasema Paul Schiff Berman, profesa wa sheria wa Chuo Kikuu cha George Washington.

Kanuni za Marekani kuhusu sheria ya uchaguzi, inasema mtu yeyote "anayelipa au kujitolea kulipa au kukubali malipo - kwa ajili ya kujiandikisha kupiga kura au kupiga kura" anaweza kutozwa faini ya dola 10,000 au kifungo cha miaka mitano jela.

"Pesa zake ziko kwa ajili ya wapigakura waliojiandikisha tu, kwa hivyo nadhani anakwenda kinyume na sheria hii," anasema Berman.

Idara ya Sheria ya Marekani ilikataa kutoa maoni.

"Hoja ya kuvunja kanuni inaweza kuwa dhaifu, kwa sababu hakuna anayelipwa moja kwa moja ili kujiandikisha au kupiga kura," anasema mwenyekiti wa zamani wa Tume ya Shirikisho ya Uchaguzi (FEC), Brad Smith.

"Hawalipi watu kujiandikisha kupiga kura. Anawalipa ili kutia saini ombi lake, anataka waliojiandikisha tu kupiga kura, kutia saini ombi hilo. Kwa hiyo nadhani yuko sawa hapa," anasema.

Lakini profesa wa sheria za uchaguzi katika Chuo Kikuu cha Northwestern aliiambia BBC lengo la pesa hiyo kutolewa ni muhimu.

"Naelewa kwa baadhi ya wachambuzi kuwa sio kinyume cha sheria, lakini lengo moja liko wazi, kushawishi watu kujiandikisha kupiga kura kwa njia ambayo ina shida kisheria," anasema Michael Kang.

Adav Noti kutoka kituo cha Campaign Legal Center, anasema mpango wa Musk "unakiuka sheria ya shirikisho na uko chini ya kosa la kiraia au jinai kwa mujibu wa Idara ya Haki."

"Ni kinyume cha sheria kutoa pesa kwa masharti kwamba wapokeaji wawe wamejisajili kama wapiga kura," anasema Noti.

Profesa wa sheria za katiba Jeremy Paul, kutoka Chuo Kikuu cha Northeastern anasema katika barua pepe kwa BBC kwamba Musk anatumia mwanya wa kisheria.

Ingawa kuna hoja kwamba pesa hizo zinaweza kuwa kinyume cha sheria, "lakini zinatolewa kwa mtindo wa kuizunguka sheria" na anaamini kesi hiyo itakuwa ngumu mahakamani.

Musk, bilionea mfuasi kindakindaki wa rais wa zamani Donald Trump, alitangaza Jumamosi iliyopita kuwa atatoa dola milioni moja kila siku hadi uchaguzi ufanyike kwa mpiga kura wa jimbo moja ambaye bahati nasibu ikichezeshwa itamwangukia .

Utoaji wa fedha hizo kutoka kwa mtu tajiri zaidi duniani ni jambo ambalo halijawahi kutokea kwa miaka mingi nchini humo.

Musk alitangaza tuzo za kila siku ya dola milioni katika mkutano wa hadhara wa Trump huko Harrisburg na Pennsylvania, Jumamosi iliyopita na siku hiyo mshindi wa kwanza akatangazwa kuwa ni John Dreher.

Wapigakura wanaweza kufanikiwa kupata zawadi kwa kusaini ombi la kuunga mkono uhuru wa kujieleza au wa maoni na haki ya kumiliki na kubeba silaha inayoendeshwa na Musk's America PAC.

Ni kampeni inayotumia mamilioni kumuunga mkono Trump ikiwa ni pamoja na kugharamia ziara za nyumba kwa nyumba katika majimbo ambayo yanaonekana kuwa yeyote kati ya Donald Trump wa Republican na Kamala Haris wa Democrat anaweza kushinda . Marekani wakiyaita 'swing states'.

Wapigakura katika majimbo ya Pennsylvania wangepokea dola milioni Jumapili na Jumatatu, na katika siku 15 zijazo watu waliotia saini PAC ambayo inasisitiza uhuru wa maoni na kumiliki silaha wa majimbo ya Pennsylvania, Georgia, Nevada, Arizona, Michigan, Wisconsin na North Carolina watafuata kupokea chao.

Wakili wa masuala ya uchaguzi Rick Hasen, anasema katika blogu yake kuwa mpango wa hivi sasa wa Musk ni kinyume cha sheria, akisema kuwa unakiuka sheria ya shirikisho inayopiga marufuku "kulipa au kutoa, ama kulipa au kukubali malipo kwa kusajili kupiga kura. Tena ni kinyume cha sheria.

Gavana wa Democrat wa Jimbo la Pennsylvania, Josh Shapiro, anamkosoa Musk na zawadi hiyo, akisema bilionea huyo ana haki ya kutoa maoni yake, "lakini anapoanza kuingiza aina hii ya kugawa pesa katika siasa, ni jambo linalozua maswali mazito ambayo watu lazima waangalie.

Mwekezaji bilionea Mark Cuban, ambaye amefanya kampeni katika wiki za hivi karibuni kwa Kamala Harris, anasema:

"Ikiwa mpango huo utafanya kazi au la ni jambo jingine. Na mpango huo unaweza hata kukupa matokeo tofauti na uyatakayo," aliiambia CNBC.

Musk amejibu ukosoaji huo, akisema Democratic na wafadhili wao wamefadhili mipango kama hiyo hapo awali.

Kwenye mtandao wa X au twiter, aliweka chapisho linalosema bosi wa Meta, Mark Zuckerburg" alifanya vivyo hivyo mwaka 2020."

Zuckerburg alichangia dola milioni 400 katika uchaguzi wa 2020 lakini pesa hiyo ilitolewa kwa mashirika mawili yasiyoegemea upande wowote ili kusaidia vifaa vya upigaji kura kwa njia ya posta. Haikutolewa moja kwa moja kwa wapigakura.

Huko nyuma Democratic, kiliwahi kuwekeza katika mipango ya kuongeza wafuasi, kwa kampeni ya usajili wa wapigakura ya dola milioni 25 katika uchaguzi wa katikati ya muhula wa Marekani wa 2022.

Lakini pesa hizo hazikutolewa moja kwa moja kwa wapiga kura. Zilikuwa ni za mipango ya kuwahimiza wapigakura kujiandikisha na zilitolewa kwa walioajiriwa kwenye kampeni za nyumba kwa nyumba, na kwa matangazo ya televisheni na mtandaoni.

"Ni halali kuwalipa watu kwenda kusajili wapiga kura, lakini huwezi kuwalipa watu moja kwa moja kujiandikisha," anasema Prof. Kang.

***BBC SWAHILI, FORBES***





# Mabaraza ya maabara, famasia yapigwa msasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge na Masuala ya Ukimwi imeyataka mabaraza ya maabara na famasia kuzingatia ubora wa huduma na mafunzo yanayotolewa kwa wataalamu wa kada hizo.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Bernadetha Mshashu, alitoa kauli hiyo baada ya kuwasilishwa taarifa ya mabaraza ya maabara na ukunga kwenye kikao cha kamati hiyo jijini hapa.

"Vipimo vya maabara ni muhimu lakini pia watoa dawa au wafamasia wanaotoa dawa bila karatasi ya daktari si sawa mnapaswa kuliangalia hilo kwani huweza kusababishia mgonjwa usugu wa dawa mwilini na kuleta athari," alisema.

Alipongeza mabaraza ya maabara na famasia kwa kuwa na mafunzo endelevu kwa wataalamu yatakayosaidia kuzingatia kanuni, sheria na miiko ya taaluma zao.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alisema serikali imeamua kuweka mifumo ambayo itaweza kusimamia na kufanya uchunguzi kwenye maabara juu ya vipimo vinavyofanyika maabara moja na nyingine na kuhakikisha matokeo ambayo mgonjwa ataambiwa maabara moja ni hayo hayo atakutana nayo katika maabara nyingine.

"Mnyororo wa tiba unaanzia maabara na famasi ni sehemu muhimu sana ni lazima upitie famasi ili uweze kupewa dawa tiba, hivyo kuangalia msingi wa maabara na kuzidi kuboresha huduma za maabara ni kitu cha muhimu sana," alisema.

Aidha, Waziri Mhagama, alisema maabara ya Taifa imepewa hadhi ya kuwa kituo muhimu cha kutoa mafunzo ya ulinzi na usalama wa vimelea hatarishi ili kuongeza usalama kwa afya za wananchi.



**Vipimo vya maabara ni muhimu lakini pia watoa dawa au wafamasia wanaotoa dawa bila karatasi ya daktari si sawa mnapaswa kuliangalia hilo kwani huweza kusababishia mgonjwa usugu wa dawa mwilini na kuleta athari.**

# Mkandarasi akwama kukabidhi ofisi Tume ya Madini Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Nishati na Madini imekagua ujenzi wa Makao Makuu ya Tume ya Madini na kumwagiza mkandarasi kukabidhi jengo ndani ya miezi miwili ili watumishi wafanye kazi kwenye mazingira rafiki.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. David Mathayo, alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo jijini hapa baada ya kushindwa kukabidhi jana kutokana na kutokamilika.

Dk. Mathayo, alisema kwa kipindi kirefu, watumishi hao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa ofisi na kusababisha kushuka kwa utendaji kazi.

"Tunataka mkandarasi kuhakikisha katika kupindi cha miezi miwili ijayo unakabidhi jengo kwa Kamati ya Bunge likiwa limekamilika kwa asilimia 100 ili watumishi wote wa Tume ya Madini waweze kukaa sehemu moja na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi na kuongeza ufanisi wao," alisema.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, aliishukuru kamati hiyo kwa ushirikiano mzuri na kutoa ushauri unaosaidia kuchochea kukua kwa sekta ya madini.

Aliahidi wizara hiyo itatekeleza maelekezo ya kamati hiyo na kufuatilia miradi yake ili ikamilike kwa wakati.

Awali, Kaimu Mtendaji wa Tume hiyo, Mhandisi Ramadhani Lwamo, alisema mradi huo wa ghorofa tatu ulitakiwa kukamilika na kukabidhiwa jana (Oktoba 22, mwaka huu) na kwamba bado ujenzi wake haujakamilika na lipo hatua za umaliziaji.

Akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya mradi huo, Msanifu Majengo kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Mhandisi Vilumba Sanga, alisema hadi sasa mradi umefikia asilimia 93.

Sanga, alisemaa maeneo yanayoendelea na ujenzi ni pamoja na uzio, ufungaji wa madirisha na upigaji rangi nje na ndani.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, akiongoza kikao cha kamati hiyo bungeni, Dodoma jana walipokutana na uongozi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kulia kwake ni Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadau kujadili utendaji uchukuzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa sekta ya uchukuzi wanatarajia kukutana kwa siku tatu mkoani Arusha kujadili na kufanya tathmini ya utendaji wa sekta hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alisema hayo juzi wakati akizungumzia mkutano wa 17 wa kutathmini utendaji wa sekta ya uchukuzi (JTSR) kwa mwaka 2023/24.

Kahyarara, alisema mkutano huo umepangwa kufanyika kuanzia leo hadi Jumamosi jijini Arusha, unaratibiwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha uchumi nchini kupitia sekta hiyo.

Alisema mkutano huo utajadili utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa 16 wa JTSR na kuja na mipango ya maendeleo ya sekta ya uchukuzi.

"Mkutano umelenga kukuza, kuimarisha na kurahisisha ufanyaji biashara nchini kupitia maboresho katika Sekta ya Uchukuzi, kwa kushirikisha mawazo na maoni ya wadau ambao ni serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuboresha utendaji wa sekta ya uchukuzi ambayo ni muhimu kwa uchumi wa taifa," alisema.

Alisema mkutano huo pia utapokea mawasilisho ya utendaji kutoka taasisi za uchukuzi kuhusu utendaji, mafanikio, fursa zilizoko na taarifa ya kisera ya sekta hiyo.

"Pia watapata majibu ya changamoto zinazokabili sekta ya uchukuzi, hasa zile zinazohusiana na miundombinu, usafirishaji, na urahisishaji wa biashara ndani na nje ya nchi," alisema.

Prof. Kahyarara, alisema wizara hiyo imeendelea kutekeleza kwa mafanikio miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Wizara hususani miradi ya maendeleo ya kielelezo ambayo ni ujenzi wa Reli ya Standard Gauge, uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania, ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu, uboreshaji wa Bandari nchini na ukarabati wa miundombinu ya usafiri kwa njia ya reli.





# Wafugaji waanza kuingiza mifugo Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya wafugaji wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wanadaiwa kupewa taarifa potofu kuwa serikali imeruhusu kuchungia mifugo kwenye Bonde la Ihefu lililoko Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kusababisha kukithiri kwa uharibifu wa mazingira.

Taarifa hizo zinadaiwa kusababisha wafugaji wengine kutoka maeneo mengine nchini kuanza kusafirisha mifugo yao na kuiingiza ndani ya bonde hilo hasa kipindi hiki cha kiangazi hali ambayo inahatarisha kutoweka kwa ikolojia ya hifadhi.

Mkuu wa Hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Ming'ataki, aliyasema hayo juzi wakati akizungunza na waandishi wa habari kuhusu hatua zinazochukuliwa kunusuru hifadhi hiyo.

Ming'ataki, alisema serikali haijaruhusu mifugo kuingizwa ndani ya hifadhi hiyo kwa kuwa bonde hilo ni muhimu kwa taifa kwa uzalishaji maji kwa matumizi ya viumbe hai na uzalishaji umeme katika mabwawa ya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere.

Alisema taarifa hizo za uzushi zimekuwa zikiibuliwa na wafugaji kwa lengo la kutaka wawe wengi katika bonde hilo ili iwe vigumu kwa serikali kuwadhibiti.

"Tumefanya doria ndani ya hifadhi, tulipofanya doria ya angani tumebaini makundi mengi ya mifugo yameingizwa ndani ya hifadhi na mengine yako eneo ambalo haliingiliki kirahisi, wengine tukiwakamata na kuwahoji, wanasema wameambiwa serikali imewaruhusu jambo ambalo sio kweli," alisema.

Ming'ataki, alisema uongozi wa hifadhi hiyo unaendelea na mikakati kudhibiti mifugo hiyo, kuimarisha ujirani mwema na vijiji vinavyoizunguka na kujadiliana na wafugaji.

Aliwaomba viongozi wa serikali za vijiji kutoa elimu kwa wananchi ili wasiingie ndani ya hifadhi na kufanya shughuli za binadamu ambazo zinahatarisha uwepo wa hifadhi.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Barick Julius, aliwataka wafugaji kuheshimu sheria za nchi kwa kuepuka kuingiza mifugo ndani ya hifadhi, la sivyo watakamatwa na kuchukuliwa hatua.

Julius, alisema serikali imehifadhi bonde hilo kutokana na umuhimu kwenye ikolojia ya hifadhi hiyo na uzalishaji maji kwa ajili ya shughuli nyingine.

Alisema chama hicho hakitakuwa tayari kumtetea mfugaji ambaye atakamatwa kwa kuingiza mifugo kwenye hifadhi hiyo na maeneo mengine yaliyopigwa marufuku na serikali.

"Hatuungi mkono mifugo kuingizwa hifadhini, wafugaji wazingatie sheria za nchi na wasikubali kutumika vibaya na mtu yeyote maana wao ndio watakaoumia mifugo yao ikikamatwa," alisema Barick.

Mtemi Njile Luneula, alisema taarifa kuwa serikali kuwaruhusu kuingiza mifugo hifadhini wamekuwa wakizisikia mitaani na kwamba hazina ukweli.

Luneula, alizifananisha taarifa hizo na propaganda ambazo zimekuwa zikiibuliwa na baadhi ya watu wenye lengo la kupata umaarufu kwa wafugaji na kusababisha migogoro kati yao na serikali.



Wamachinga wakiendelea na biashara zao kwenye barabara ya mabasi ya mwendokasi, Mbagala Dar es Salaam jana, eneo ambalo lilizuiwa kufanywa biashara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanafunzi wanufaika kwa kilimo, mazingira

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI zaidi ya 1,600 wa shule za sekondari mkoani hapa wamenufaika na programu ya nadharia na vitendo kupitia klabu za kilimo na uhifadhi wa mazingira inayoendeshwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) kupitia program ya Forest and Farm facility (FFF).

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa MVIWATA wa Mkoa wa Njombe, Nobert Mwalongo katika Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Chakula yanayofanyika Shule ya Sekondari Ninga wilayani Njombe.

Mwalongo, alisema programu hiyo ni muhimu kuendeleza na kuimarisha maarifa ya vijana na wanafunzi katika mfumo wa chakula unaoweza kuwapa lishe bora na utunzaji wa mazingira.

"Tumegundua suala la elimu wanafunzi kujitegemea hususan katika nchi ambayo kwa upana wake imetawaliwa zaidi na wakulima, tumeona ipo haja ya kushirikisha wanafunzi," alisema Mwalongo.

Alisema shule hizo kupitia klabu zao, zimeshiriki katika shughuli za utunzaji wa mazingira na kilimo cha bustani za mboga kwa kutumia njia za kiikolojia baada ya MVIWATA kuwezesha vifaa ikiwamo mbegu za mboga, miti na vifaa vya kumwagilia.

"Utekelezaji wa programu ya uanzishaji wa klabu za kilimo na mazingira ulianza na wilaya mbili (Ludewa na Njombe) na kuzifikia shule 15 zenye wanachama 724," alisema na kuongeza kuwa:

"Jitihada za ushirikishaji wa wanafunzi zimekuwa zikiendelea na sasa zimeongezeka shule tatu, mbili Wilaya ya Wanging'ombe na moja Ludewa."

Mwalimu Mkuu Shule ya Sekondari Ninga, Geofrey Mgina, alisema shule hiyo imeanzisha mradi wa matunda, miti ya biashara, mazao ya chakula na bustani ya mboga kwa ajili ya kuwaongezea kipato na lishe kwa wanafunzi.

Mjumbe wa Bodi ya MVIWATA, Mendrad Nziku, alizishukuru shule ambazo zimekubali kupokea mradi huo na elimu wanayoipata wanafunzi hao itawasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Baadhi ya wanafunzi, akiwamo Daniel Kifyulilo wa Shule ya Sekondari Ninga, alisema progamu hiyo imewasaidia kupata elimu ya kuandaa bustani za mboga na kuimarisha lishe zao.

# 23,000 wapatiwa matibabu hospitali rufani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAGONJWA zaidi ya 23,000 wamepatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Gilbert Kwesi, katika uzinduzi wa huduma ya uchunguzi wa magonjwa ya mfumo wa chakula.

Dk. Kwesi, alisema kati ya wagonjwa hao walipatiwa matibabu kwa kipindi hicho, wa dharura na mahututi walikuwa 1,322.

Alisema magonjwa hayo ya mfumo wa chakula mchanganyiko yamekuwa yakiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa.

Alisema kwa kipindi hicho, wagonjwa 566 wamefanyiwa uchunguzi na kutibiwa.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka baada ya kuzindua huduma hiyo, aliwataka watumishi wa hospitali kuendelea kutoa huduma bora na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.

"Fanyeni kazi kwa kuzingatia maadili, tembeeni kifua mbele kwa sababu serikali inaendelea kuhakikisha mnafanya kazi katika mazingira rafiki na kuridhisha pamoja na kutatua matatizo yenu ya kimaslahi," alisema Mtaka.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Judica Omary, alitoa rai kwa watoa huduma hao kuongeza ufanisi ili maboresho ya vifaa tiba yaweze kuleta tija.



# Mwinyi, madaktari bingwa India wateta

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar inahitaji kuungwa mkono kwenye utaalamu, miundombinu na kuwajengea uwezo watendaji wa sekta ya afya ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na timu ya madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Umoja wa Madaktari Bingwa wenye asili ya India wanaoishi Marekani (GAPIO) kuelezea dhamira yao ya kushirikina na serikali kuimarisha sekta ya afya katika maeneo mbalimbali.

Alisema Serikali ya Zanzibar inaendelea na ujenzi wa miundombinu ikiwamo hospitali za wilaya na vituo vya afya kwa maeneo ya Unguja na Pemba ili kuhakikisha wananchi wanapata matibabu bora.

Hata hivyo, alisema bado kuna pengo linalohitaji kufanyiwa kazi ili kufikia malengo ikiwamo, upatikanaji wa vifaa tiba na dawa za kutosha, rasilimali watu, fedha hasa katika usimamizi wa bima ya afya na miundombinu kwenye sekta ya afya.

Akizungumzia kuanzishwa kwa bima ya afya kwa wenyeji na wageni wanaoingia nchini, Dk. Mwinyi alisema inasaidia fedha za uendeshaji kwa sekta ya afya akitolea mfano watalii 18 ambao wamenufaika nayo.

Alisema serikali inakusudia kuimarisha huduma za bima ya afya kwa njia ya kidigitali ili kurahisisha wageni kupata huduma hiyo hata wakiwa nje ya Zanzibar.

Alisema kuna haja ya kuangalia mfumo mzima wa sekta ya afya licha ya kujengwa hospitali 11 za wilaya, bado kuna changamoto zimejitokeza ikiwamo uhaba wa wataalamu kwenye hospitali hizo, vifaa tiba na dawa na teknolojia ndogo.

Kuhusu rasilimali watu, Rais Mwinyi, aliwataka wataalamu hao kuangalia zaidi uwezekano wa kuwawezesha utaalamu na mfumo wa uendeshaji wa sekta ya afya, Zanzibar.

Aliwahakikishia madaktari hao kuwa serikali ipo tayari kushirikiana nao kwa kuandaa mazingira rafiki ya kufanyakazi pamoja na ukaribu zaidi kwa kuwa na mipango ya muda mfupi, wakati na muda mrefu ili kuimarisha ushirikiano baina yao kupitia Wizara ya Afya na GAPIO.

Mratibu wa ujio wa madaktari hao kutoka Hospitali ya Apolo ya Dar es Salaam, Dk. Nazir Arab, alisema lengo ya taasisi yao ni kusambaza madaktari zaidi ya 1.4 milioni duniani, Tanzania na Zanzibar ikiwa miongoni.

Alisema GAPIO inawakilishwa katika nchi 57 duniani hasa kwa mataifa ya mashariki ya mbali, kusini mashariki mwa bara Asia na Afrika ili uimarisha sekta ya afya duniani.

Timu hiyo ya madaktari bingwa 20 ikiongozwa na Prof. Sanku Rao wakifuatia na Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya, Dk. Salim Slim na timu ya watendaji ya wizara hiyo, watakuwa na vikao vya pamoja vya kubainisha maeneo ya ushirikiano hasa katika magonjwa na wataalamu wa upasuaji wa maradhi ya moyo, matumbo ya kawaida na mifupa.



Magari yakiwa kwenye foleni katika barabara ya kuelekea Chamazi Dar es Salaam jana, mashuhuda walisema ilisababishwa na baadhi ya madereva wa daladala kushusha na kupakia abiria barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Ujumbe wa Marekani watua Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema amani ni muhimu kwa nchi kuendeleza na kukuza uchumi kupitia biashara ya uwekezaji.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake wakati alipokutana na ujumbe uliongozwa na Ofisa Mwandamizi wa Kamati ya wataalamu ya uhusiano wa Mambo ya Nje, Heather Flynn kutoka Bunge la Senate la Marekani.

Alisema Zanzibar inakaribisha uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wenye uwezo kwa nia ya kuharakisha maendeleo ya ukuaji wa uchumi wake.

Alisema ni muhimu kuwapo amani ya kweli ambayo itasaidia kuleta na kujenga imani kwa wawekezaji ambao ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Othman ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, alisema chama chake chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kitaendelea kupigania mageuzi ya kidemokrasia nchini ambayo ni muhimu kuleta maendeleo na kulinda haki za kidemokrasia nchini kwa kuzingatia maslahi ya wananchi na taifa.

Alisema wawekezaji wanahitaji kwenda kwenye taifa lenye amani na utulivu wa kweli. Othman, alisema ushirikano mkubwa uliopo na nchi ya Marekani umesaidia kusukuma mbele demokrasia na utawala bora kupitia misaada kutoka taasisi na mashirika ya nchi hiyo.

Alisema kwamba serikali ya Zanzibar yenye muondo wa umoja wa kitaifa pamoja na wananchi inafahamu juhudi za misaada inayotolewa na Marekani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

# Tamasha la utalii, uwekezaji kulindima kesho kutwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema Tamasha la Utalii na Uwekezaji Zanzibar litaviweka visiwa hivyo katika ramani ya kuwa kitovu cha utalii duniani.

Alisema tamasha hilo litaanza siku tatu zijazo, hasa ikizingatiwa kuwa hivi karibu Zanzibar imetambulika na duniani kuwa sehemu nzuri ya kufanya matamasha.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa, wakati akizungumza katika hafla ya maonesho ya chakula cha asili ya Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za tamasha hilo linalotarajiwa kufanyika kesho kutwa na kufunguliwa na Rais Dk Hussein Ali Mwinyi.

Alisema wizara hiyo itahakikisha inaendeleza matamasha kwa sababu ni fursa za kiuchumi, utalii na uwekezaji.

Alisema tamasha hilo linatarajiwa kujumuisha wageni kutoka nchi mbalimbali duniani ikiwamo Ujerumani, Ufaransa na Uingereza.

"Hii inaonesha jinsi gani Zanzibar hivi sasa ubora wake unazidi kuwa mkubwa na watu wengi wanaona umuhimu wa kuja kuangalia fursa na kujitangaza," alisema Soraga.

Waziri huyo, alisema maandalizi yake tamasha hilo yanaendelea vizuri.

Alisema chakula cha asili ya Zanzibar ni miongoni mwa vitu vitakavyotangazwa katika tamasha hilo kwa vile ni tofauti na vyakula vya mataifa mengine.

Kamishna wa Utalii Zanzibar, Wilfed Shirima, alisema tamasha hilo litasaidia kutangaza utalii wa Zanzibar na kuleta watalii wengi kutoka sehemu mbalimbali za duniani kuja kujionea fursa zilizopo.

Shirima, alisema visiwa vya Zanzibar vina fursa nyingi katika uwekezaji, ikiwamo utalii wa fukwe, halali wa kihistoria, asili na utamaduni.

Mkurugenzi wa Shamba la Msonge, Dk. Mwatima Abdallah Juma, alisema kilimo hai kina fursa kubwa katika soko la utalii na watalii wanajifunza mambo mengi katika vyakula vya asili na mapishi yake.

HABARIKIMATAIFA

# Benki Kuu Afrika zashauriwa kutafuta fedha kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Benny Mwaipaja, WASHINGTON D.C**

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-maamry Mwamba, ametoa wito kwa Benki Kuu za Nchi za Afrika, kuweka mipango na mikakati ya kutafuta fedha kupitia vyanzo mbalimbali ikiwamo sekta binafsi kwa ajili ya kukabiliana na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi katika nchi hizo.

Dk. Mwamba alitoa rai hiyo wakati akishiriki mjadala kuhusu wajibu wa Benki Kuu za nchi za Afrika kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 30 tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Macroeconomic and Financial Management of Eastern and Southern Africa (MEFMI), mjadala uliofanyika kando ya mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), jijini Washington D.C, nchini Marekani.

Alisema mbinu mahususi ikiwamo uanzishwaji wa hati fungani za kijani zenye lengo la kuvutia uwekezaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na kusimamia ipasavyo taasisi za fedha kuwekeza kwenye kilimo kwa kutoa mikopo, zitasaidia kukuza uchumi wa nchi hizo za Afrika na maendeleo ya watu wake.

Dk. Mwamba alibainisha katika tukio hilo lililowakutanisha mawaziri wa fedha, makatibu wakuu na magavana wa Benki Kuu kutoka nchi za Afrika, alisema mabadiliko ya tabianchi yameziathiri nchi nyingi ikiwamo Tanzania na upatikanaji wa fedha kwa njia shirikishi katika kukabiliana na athari hizo kutaimarisha uchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MEFMI, Dk. Louis Kasekende, alisema kuwa taasisi yake imejipanga kuwawezesha wanachama wake kuweka mipango ya pamoja ya kutafuta fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa uhimilivu wa madeni ya nchi za Afrika.

Washiriki wengine katika mkutano huo kutoka Tanzania, walikuwa Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Sera za Uchumi kutoka Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba.



Naibu Rais Rigathi Gachagua. **PICHA: MTANDAO**

# Ruto apuuzia uamuzi wa Mahakama

**NAIROBI, Kenya**

WAKILI wa Rais William Ruto, amesema mteja wake, hajaridhishwa na uamuzi wa Mahakama ya Juu, kupinga kuondolewa kwa Naibu Rais Rigathi Gachagua, akisema haina mamlaka ya kusikiliza, kuamua kesi za kupinga kuondolewa kwa Gachagua madarakani.

Wakati huo huo, Naibu Rais aliyeondolewa mamlakani, Rigathi Gachagua, jana, amehudhuria kikao cha Mahakama Kuu, zikisikilizwa kesi mbili za kupinga kuondolewa kwake mamlakani.

Gachagua alifika katika Mahakama ya Milimani jijini Nairobi, akiwa na msafara wa magari sita akiandamana na Mbunge wa Embakasi ya Kati Benjamin Gathiru, maarufu Major Donk, aliyekuwa Katibu Mkuu wa United Democratic Alliance (UDA), Cleophas Malala na mawakili kadhaa.

Kulikuwa na maafisa wengi wa usalama katika majengo ya mahakama na hata ndani ya mahakama.

Walipofika mbele ya majaji Eric Ogola, Anthony Mrima na Freda Mugambi, mawakili wa Gachagua, wakiongozwa na Wakili Mkuu Paul Muite, walisema hawakuwa kortini kwa hiari yao.

Mahakama ilieleza kuwa faili za kesi zilitumwa kwa Jaji Mkuu, Oktoba 18 na Naibu Jaji Mkuu, Philomena Mwilu akateua majaji kusikiliza kesi hizo.

Jaji Mrima alisema kesi hizo, ziliwasilishwa kupitia mtandao na majaji wakaagiza zitajwe jana.

Jopo la majaji watu likiongozwa na Jaji Eric Ogola pia linajumuisha majaji Anthony Mrima na Freda Mugambi lilichanguliwa na Naibu Jaji Mkuu Mwilu, kusikiliza kesi zote zenye kuhusu kuondolewa madarakani kwa Gachagua.

Jana, kupitia Wakili Adrian Kamotho, Ruto anadai kuwa Mahakama ya Juu zaidi pekee ndiyo yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hizo.

Kulingana na Rais William Ruto, mahakama inafaa kutupilia mbali kesi hizo akidai kuwa zimewasilishwa kinyume cha sheria na ni utumiaji mbaya wa mchakato wa mahakama.

Rais Ruto ameongeza kuwa kesi dhidi ya Rais au mtu anayetekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais katika kipindi cha uongozi wake kuhusiana na jambo lolote lililofanywa au kutofanywa chini ya sheria ya Katiba ya Kenya 2010, haziwezi kufunguliwa katika mahakama yoyote tu.

***BBC/TAIFA LEO***

## Silaa aagiza mnara upandishwe hadhi kupata mtandao 4G

**Na Thobias Mwanakatwe, MANYONI**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amemwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo kuupandisha hadhi mnara uliojengwa katika Kijiji cha Hika, Kata ya Makuru, wilayani Manyoni ili wananchi waweze kupata mtandao wa intaneti wa 3G hadi 4G.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho katika siku ya kwanza ya ziara yake ya siku tano mkoani Singida baada ya kuzindua mnara wa mawasiliano ya simu uliojengwa na serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) uliojengwa kwa Sh. milioni 272.

"Naomba kutumia fursa hii kwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kati ya maelekezo aliyonipa wakati akiniapisha ni kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano namwelekeza Katibu Mkuu ahakikishe kwa haraka sana mnara huu unapandishwa hadhi na unapata mtandao wa 3G na 4G ili wananchi nao waweze kupata intaneti," alisema.

Alisema wananchi wa kata hiyo zaidi ya 24,000 wanatakiwa kupata mtandao wa intaneti ili hata wakisikia Rais Dk. Samia anazungumza sehemu fulani waweze kuingia kwenye mtandao na kumsikiliza kupitia simu janja.

"Tunataka wananchi wa kata hii waanze kupunguza simu janja wapate mtandao wa intaneti wakisikia Dk. Samia anaongea mahali na wenyewe waingie kwenye mtandao wamwone na pia wakisikia Yanga ipo Uwanja wa Taifa wakimshughulikia mtu na wenyewe waangalie matokeo ,live' kupitia mtandao," alisema.

Meneja wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Agustino Mwakyembe, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Moremi Marwa, alisema ujenzi wa mnara huo wenye urefu wa mita 60 ulianza baada ya kutiwa saini makubaliano Machi 16, 2021 na ujenzi kukamilika Juni 15, 2022.

Alisema mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 272 unatumia teknolojia ya 2G ambao unawezesha wananchi kupiga na kupokea simu za sauti huku wakitumia ujumbe mfupi kwa wakati mmoja (sms). Mwakyembe alisema TTCL imeanzisha mtandao wa mawakala wanaotoa huduma za kifedha kupitia T-PESA pamoja na mawakala wenye jukumu la kuuza vocha za muda wa maongezi na kusajili laini za simu.

HABARI MICHEZO

# MASHUJAA FC YAANIKA SIRI YA USHINDI, YAITISHA SIMBA

Na Somoe Ng'itu

BAADA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KenGold hapo juzi, Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah 'Bares', amesema siri ya matokeo hayo imetokana na wachezaji wake kufanya mazoezi ya kufunga zaidi.

Mashujaa sasa imefikisha pointi 12 na kupaa hadi nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bares alisema alibaini wachezaji wake kupoteza nafasi wanazotengeneza katika michezo iliyopita na kabla ya kuivaa Ken Gold, walilazimika kufanya mazoezi ya kufunga kwa muda mrefu.

Bares aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuongeza umakini katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na kutimiza malengo ya kuzibakisha pointi tatu muhimu nyumbani.

"Kwanza tunamshukuru Mungu, tujipongeze kupata alama tatu, tulikuwa tunatengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, kabla ya mechi hii tulifanya sana mazoezi ya ufungaji, naona vijana wamefanya kazi ile tuliyoitarajia, " alisema Bares.

Kocha huyo alisema ushindi huo utawasaidia kuingia wakiwa imara kuwakabili Simba ambao wanawafuata wakiwa wametoka kupoteza dhidi ya watani zao, Yanga.

Aliongeza kuwa licha ya kupata ushindi, mechi hiyo haikuwa rahisi huku akiwapongeza wapinzani wao KenGold kwa kusema wanakikosi kizuri na imara.

Naye Mchezaji Bora wa mechi hiyo, Ismail Mgunda, ambaye alifunga mabao mawili katika ushindi huo alisema siri ya kufanya vizuri ilitokana na wachezaji kufuata vema maelekezo ya benchi la ufundi.

Mgunda alisema kila mchezaji aliyepata nafasi katika mechi hiyo alitimiza vizuri majukumu yake kwa sababu walizihitaji zaidi pointi tatu za nyumbani.

Alisema mechi hiyo haikuwa rahisi kwa sababu KenGold pia ina kikosi imara na kiliingia katika mchezo huo kikiwa na morali ya kupata ushindi wa nyumbani kwao.

"Mchezo haukuwa rahisi, KenGold ni timu nzuri, mimi na wachezaji wenzangu tulipambana zaidi kuhakikisha tunapata ushindi, tulijiandaa kuhakikisha tunawapa furaha mashabiki wetu,...hii ni tuzo yangu ya kwanza, ninaamini nitaendelea kujituma, tutarajie mengi makubwa," Mgunda alisema.

Mgunda pia alitoa pasi ya mwisho ya bao lingine lililofungwa na Julius Kamoga, zikiwa zimebakia dakika nne kabla ya mechi hiyo kumalizika.

Mashujaa sasa inajiandaa kuikaribisha Simba katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Oktoba 31, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kulia), akipiga hesabu za kumtoka mchezaji wa Tanzania Prisons, Dotto Shabani, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya jana. Simba ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Mlandege yaota kupanda kileleni

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

LICHA ya kugawana pointi na Mwembe Makumbi City FC, Kocha Msaidizi wa Mlandege, Sabri China, amesema bado malengo ya timu yake ni kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar wakiwa kileleni, imeelezwa.

Mlandege imelazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, Mwembe Makumbi City katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex juzi jioni.

Kwa matokeo hayo, Mwembe Makumbi City yenye pointi 16 inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakati Mlandege FC wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 13 kibindoni.

Mchezo huo uliokuwa na ushindani wa dakika zote, ulihudhuriwa na idadi kubwa ya mashabiki ukilinganisha na mechi nyingine zilizochezwa msimu huu katika ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Akizungumza na gazeti hili jana, China alisema walipanga kuvuna pointi tatu lakini mipango yao haikutimia kutokana na ushindani na ugumu uliokuwapo katika mchezo huo.

China alisema bado wataendelea kujiimarisha kuhakikisha hawapotezi pointi katika michezo inayofuata na hatimaye kukaa kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Mchezo huo haukuwa mgumu uwanjani kutokana na uzoefu tuliokuwa nao katika Ligi Kuu, lakini wachezaji wangu walishindwa kuzisoma vyema mbinu za wapinzani hali iliyopelekea kucheza kwa hasira na kupoteza umakini," alisema China.

Aliongeza licha ya kutopata alama tatu katika mchezo bado wanaimani watatinga kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo kwa sababu watafanya vizuri michezo inayofuata ili kukamilisha mzunguko wa kwanza.

"Hatukuwa na sababu ya kushindwa kuondoka na alama tatu katika mchezo huu, wachezaji walishindwa kwenda na kasi ya uchezaji wa nguvu dhidi ya wapinzani wetu na hatima yake tuliingia katika mfumo wao, tumekuja kusawazishiwa bao la pili dakika za nyongeza kabla ya kukamilika kwa dakika 90, hapa wachezaji hawakuwa makini hasa kucheza na muda," China aliongeza.

Alisema wanaenda kurekebisha mapungufu ili katika mechi ijayo ya raundi ya nane dhidi ya KVZ FC itakayochezwa keshokutwa wapambane kuvuna pointi tatu na kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa.

# Twiga Stars yaifuata Morocco

Na Mwandishi Wetu

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kimewasili salama Morocco tayari kwa michezo miwili ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa nchini humo.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, aliliambia gazeti hili, wachezaji wote wako katika hali nzuri na sasa wanasubiri ratiba ya michezo kutoka kwa wenyeji wao.

Shime alisema wakiwa huko wanatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki ambapo watawavaa wenyeji Morocco na nyingine itakuwa dhidi ya Senegal.

"Tumefika salama, wachezaji wote walioko katika msafara huu wako vizuri, leo (jana), jioni tutafanya mazoezi mepesi, halafu kesho (leo), tutapata ratiba kamili kutoka kwa wenyeji wetu, tunatarajia mechi mbili za kirafiki tutakazocheza zitaendelea kukiboresha kikosi chetu," Shime alisema.

Aliongeza Morocco na Senegal zote zimefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), ambazo zitafanyika mwakani, hivyo ni kipimo kizuri kwa timu yake.

Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lilisogeza mbele fainali za WAFCON, ambazo sasa zitachezwa kuanzia Julai 6 hadi 26, mwakani nchini Morocco ambapo Twiga Stars imefuzu kushiriki michuano hiyo kwa mara ya pili.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD AGOMBEWA

KLABU za Bayern Munich na Marseille zimeungana na Paris St-Germain katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26, kutoka Manchester United. ***(Tea Talk)***

### ANTONY KWA MIKOPO

KLABU ya Manchester United ipo tayari kupokea ofa za mkopo kwa ajili ya winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, wakati wa usajili wa Januari. ***(Football Insider)***

### TOTTI KURUDI UWANJANI

GWIJI wa Italia na AS Roma, Francesco Totti mwenye umri wa miaka 48, amesema huenda akarejea uwanjani baada ya kuwasiliana na klabu kadhaa za Serie A. ***(Gazzetta Dello Sport)***

### ALONSO KUONDOKA

KLABU ya Bayer Leverkusen inajiandaa kwa ajili ya kuondoka kwa kocha, Xabi Alonso, msimu ujao. ***(Bild)***

### GLOUKH AIVUTIA ARSENAL

ARSENAL, Aston Villa na Newcastle United zinanavutiwa na kiungo mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Oscar Gloukh, 20. ***(Caught Offside)***

### KILICSOY AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton inaandaa dau la pauni milioni 17 kumnunua mshambuliaji wa Besiktas mwenye umri wa miaka 19, Mturuki Semih Kilicsoy. ***(Kontraspor)***

### BARCA KUCHEZA MAREKANI

LALIGA inaomba Shirikisho la Soka la Hispania, Uefa na Fifa kuruhusu mchezo wa Barcelona dhidi ya Atletico Madrid wa Desemba kufanyika Miami nchini Marekani. ***(Mail)***

### ROVERS KUNUNULIWA

RAPA wa Marekani A$AP Rocky ni sehemu ya kundi la uwekezaji linalotaka kununua hisa za Klabu ya Tranmere Rovers kwa pauni milioni 15. ***(Sun)***

### MBEUMO ATAJWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imepania kumsajili mshambuliaji wa Brentford na Cameroon, Bryan Mbeumo mwenye miaka 25, baada ya kuanza vema msimu huu. ***(Football Insider)***

### LOPETEGUI HATAFUKUZWA

JULIEN Lopetegui hayuko katika hatari ya kufutwa kazi kama kocha wa West Ham licha ya msimu huu mbaya wa klabu hiyo. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA ATOA ONYO WACHEZAJI ARSENAL

●●● Ni kuhusu nidhamu, tangu ameanza kuinoa 2019, wamekula nyekundu 18, ikiwa ni...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amewaonya wachezaji Arsenal kwamba hawawezi kuendelea na kiwango chao cha utovu wa nidhamu.

William Saliba alikuwa mchezaji wa tatu wa Arsenal kutolewa nje kwa kadi nyekundu msimu huu alipomvuta Evanilson katika kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Bournemouth, baada ya Declan Rice na Leandro Trossard kuoneshwa mwanzoni mwa msimu huu.

Tangu Arteta alipoanza kuinoa Arsenal mnamo Desemba 2019, ‚Washikabunduki' hao wameoneshwa jumla ya kadi nyekundu 18. Hakuna timu nyingine ya Ligi Kuu England iliyooneshwa zaidi ya Kadi 13 kwa wakati huo.

Kadi nyekundu za hivi punde zilipatikana katika mechi tatu pekee ambazo Arsenal wameshindwa kushinda hadi sasa mwaka huu, na Arteta amekiri kwamba timu yake haitaweza kuwania taji la Ligi Kuu ikiwa wataendelea na hali hiyo.

"Kucheza na wanaume kumi, ni wazi kuna suala," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ukweli ni kwamba unapochambua vitendo vitatu tofauti na matokeo yake, sababu ni tofauti sana.

"Bila kujali hilo hatuwezi kuendelea kucheza na wanaume kumi hasa katika kiwango hiki, na unaona jinsi timu zote zinavyokuwa na ugumu wa kushinda mechi za soka, unapotaka kufanya hivyo dhidi ya watu kumi kwa dakika 65 kazi inakuwa karibu haiwezekani. Kwa hiyo, tunahitaji kutokomeza hilo."

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 136 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi ya leseni ya usambazaji wa gesi asilia iliyoshindiliwa kutoka kwa kampuni ya **TAN HEALTH LIMITED**, yenye ofisi yake ghorofa ya pili, Oyster Pearl Galleria, kiwanja namba 372, kitalu A, kandokando ya barabara ya Chole, eneo la Oysterbay, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam

Hivyo basi, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.


**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Huduma kwa Wteja: 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O. Box 2857, Dodoma, Tanzania
Tel: +255 26 2329002 – 4 • Fax: +255 26 2329005 • E-mail: info@ewura.go tz

# NEYMAR AREJEA UWANJANI BAADA YA MWAKA MMOJA

**RIYADH, Saudi Arabia**



NEYMAR ameonekana kwa mara ya kwanza dimbani katika kipindi cha mwaka mmoja, akitokea benchi katika kipindi cha pili cha mchezo wa Ligi ya Mabingwa Asia wakatil AFC Al Hilal ikiivaa Al Ain.

Nyota huyo wa Brazil alichukua nafasi ya Nasser Al Dawsari dakika ya 77, mara tu baada ya Salem Al Dawsari kufunga bao na kuifanya Al Hilal kuwa mbele kwa mabao 5-3.

Alikaribia kufunga bao akibadilishana pasi na Aleksandar Mitrovic ili kutengeneza nafasi kabla ya kupiga shuti lake nje kidogo ya lango.

Mchezo huo ulimalizika kwa Al Hilal kushinda mabao 5-4 baada ya Al Ain yenye maskani yake Falme za Kiarabu kufunga penalti ya dakika za mwisho.

Baada ya mchezo huo, Neymar alisema: „Ninajisikia vizuri... huwa nina timu nzuri. Nina furaha sana. Nimerejea!“.

Mchezaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain, alipata jeraha la goti wakati wa mechi ya kufuzu Kombe la Dunia ya Brazil dhidi ya Uruguay muda mfupi baada ya kujiunga na Ligi ya Saudia na alifanyiwa upasuaji Novemba mwaka jana.

Neymar alijiunga na Al Hilal Agosti 2023 akitokea PSG kwa uhamisho wa euro milioni 90, lakini alicheza mechi tano tu kabla ya kuumia.

Klabu ya zamani ya Neymar, Santos ilimpongeza mchezaji huyo kwa kurejea kwenye chapisho lake katika ukurasa wa X.

„Ilikuwa ni zaidi ya miezi 12 mbali na uwanja, na hamu kubwa ya kurudi kufanya kile anachopenda sana,“ klabu hiyo ya Brazil iliandika.

„Neymar si nyota tu. Si fikra tu. Neymar ni sawa na furaha katika soka. Kurejea kwake ni furaha ya mamilioni ya mashabiki duniani kote.“

Fowadi huyo, ambaye ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil, alikosa michuano ya Copa America ya 2024 ambayo ilinyakuliwa na Argentina.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED** kitakacho jengwa kiwanja namba P40264 eneo la Kunduchi, Salasala, Kata ya Wazo, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Huduma kwa Wteja: 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O. Box 2857, Dodoma, Tanzania
Tel: +255 26 2329002 – 4 • Fax: +255 26 2329005 • E-mail: info@ewura.go tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **TANZANIA STATES NATURAL GAS HOLDING COMPANY LIMITED** kitakacho jengwa kiwanja namba P46963, mtaa wa Kunguru, Kata ya Goba, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Huduma kwa Wateja: 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O. Box 2857, Dodoma, Tanzania
Tel: +255 26 2329002 – 4 • Fax: +255 26 2329005 • E-mail: info@ewura.go tz

HABARI MICHEZO

# MANULA AREJESHWA STARS KUSAKA TIKETI YA CHAN

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Simba, Aishi Manula, ni mmoja wa wachezaji 24 walioteuliwa kuunda kikosi cha timu ya soka, Taifa Stars, kitakachoingia kambini kucheza mchezo wa kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika mwakani.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limesema Bakari Shime, ambaye atakuwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, ameteua kikosi hicho cha wachezaji wanaocheza ligi ya ndani kwa ajili ya mchezo wa mtoano dhidi ya Sudan unaotarajiwa kupigwa kati ya Oktoba 25 hadi 27, huku marudiano yakitarajiwa kuchezwa kati ya Novemba Mosi hadi 3, mwaka huu.

Fainali za CHAN zinatarajiwa kucheza nchini Tanzania, Kenya na Uganda kuanzia Februari Mosi hadi 28, mwakani.

Hata hivyo, uteuzi wa Manula umekuja wakati kipa huyo akiwa hana namba katika klabu yake ya Simba, na si kucheza, bali amekuwa hakai hata benchi.

Mbali na Manula, wachezaji wengine wanaocheza ligi ya ndani walioitwa kwenye kikosi hicho ni Isaya Kasanga kutoka TFF Academy TDS, akiichezea pia timu ya Prisons chini ya miaka 17.

Wengine ni Antony Mpenda kutoka Azam chini ya miaka 20, Nickson Mosha (KMC), Lameck Lawi (Coastal Union), Vedatus Masinde (TMA FC inayocheza Ligi ya Champioship), Hijjah Shamte (Kegar Sugar), Abdulkaris Kiswanya (Azam chini ya miaka 20), Shekhan Khamis (Yanga), Ahmed Pipino (Magnet FC), Sabri Kondo (KVZ), Bakari Msimu (Coastal Union) na Velentino Mashaka kutoka Simba.

Wachezaji wote waliotajwa hapo juu wanaichezea pia Timu ya Taifa ya Tanzania chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes.

Wachezaji wengine ambao hawapo Ngorongoro Heroes, mbali na Manula na Kasanga ni Paschal Msindo na Adolf Mtasingwa wote wa Azam FC, David Brayson na Ismail Kada wa JKT Tanzania, Ibrahim Ame na Cyprian Ngushi wa Mashujaa FC, Charles Semfuko wa Coastal Union, Salum Ramadhani kutoka KenGold, na kinara wa mabao Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na mabao sita, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate.



Manula

# Zanzibar Marathon kuchochea uchumi

**Na Faustine Feliciane**

MSIMU wa pili wa mashindano ya Riadha ya Tigo Zanzibar Marathon unatarajiwa kufanyika Novemba 3, mwaka huu, Unguja, Zanzibar.

Mbio hizo zinatarajiwa kuchochea ukuaji wa uchumi wa buluu kutokana na kuhusisha wanariadha mbalimbali wa nje na ndani ya Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Tigo Zantel Kanda ya Zanzibar, Azizi Saidi Ali, alisema mbio hizo zitakuwa za kilomita tano, 10 na 21 na zitasaidia kuibua vipaji, kukuza uchumi na kuimarisha afya za wananchi.

„Maandalizi yote muhimu yanaendelea na yapo hatua za mwisho, tumeongeza vituo vya kujiandikisha kwa watu wanaotaka kushiriki, lakini pia kwa mwaka huu tumerahisisha usajili ambapo mtu anaweza kujisajili kwa njia ya simu," alisema Ali.

Aidha, alisema pia wameboresha zaidi mbio hizo na kuwataka wanariadha na wapenda mchezo huo kujitokeza kwa wingi kushiriki.

Mmoja wa wadau wa mbio hizo, Hussein Juma Khamis, ambaye ni mwongoza watalii Zanzibar, alisema mbio hizo zinawaongezea nafasi za kuongeza kipato.

„Wakati wa mashindano haya wageni wanaongezeka sana hapa Zanzibar...tunapata fursa ya kipato katika sekta mbalimbali," alisema Khamis.

Aidha, Anwar Ali Salim ambaye ni dereva wa magari ya watalii, alisema wanasubiri kwa shauku kubwa mbio hizo maarufu Zanzibar.

„Mbio hizi pia zinasaidia washiriki kuimarisha afya, kukimbia ni dawa, watu tujitokeze kwa wingi kushiriki," alisema Ali Salim.

Mwaka jana mashindano hayo yalifanyika kwa mafanikio makubwa na kuhusisha mamia ya wanariadha.

## Che Malone aitakatisha Simba Mbeya ikizoa tatu

INATOKA UK. 24

mabao kupitia kwa Edwin Balua aliyeingia katika dakika ya 61 kuchukua nafasi ya nahodha, Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Awali, Ateba alikaribia kuipa Simba bao la pili katika dakika ya 58 kabla ya kutolewa dakika ya 72 na nafasi yake kuchukuliwa na Steven Mukwala mabadiliko ambayo yaliongeza kasi ya mashambulizi, lakini hawakufanikiwa kupata bao lingine.

Tanzania Prisons ilijibu mapigo kwa nyakati tofauti kipindi cha pili, lakini umakini wa safu ya ulinzi ya Simba uliwanyima nafasi ya kupata bao la kusawazisha. Dakika ya 76 Mukwala alikosa bao baada ya mpira wake wa kichwa akiunganisha faulo ya Mutale kutoka juu kidogo ya goli.

Simba walifanya mabadiliko mengine dakika ya 83 baada ya kumtoa Ladack Chasambi na nafasi yake kuchukuliwa na kiungo Muzamiru Yassin, hata hivyo mabadiliko hayo hayukubadilisha matokeo.

Katika mchezo huo, Kibu ambaye alikuwa tishio kwa mabeki wa Yanga mchezo uliopita, aliendelea moto wake jana kwa kuitesa ngome ya Prisons mara kwa mara kwa dakika zote 90 za mechi hiyo.

Ushindi huo licha ya kuihakikishia Simba pointi tatu, lakini pia wamelipa kisasi cha kufungwa kwenye mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu uliopita.

Kwa matokeo hayo pia yanaifanya Prisons kubaki katika nafasi ya 12 huku Simba ikipanda mpaka nafasi ya pili nyumba Singida Black Stars yenye pointi 19, lakini ikiwa na michezo miwili zaidi.

Singida Fountain Gate inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi sawa na Simba, lakini pia ikizidiwa idadi ya mabao ya kufunga na kufungwa, Yanga ambayo jana jioni ilitarajiwa kucheza mchezo wao wa saba inashika nafasi ya nne ikiwa na pointi 15.

## Diarra atoa siri kumzuia Ateba

INATOKA UK. 24

anavyocheza, nilifahamu akipata mpira eneo lile atafanya nini.

"Nilijua ataenda kushoto, hivyo sikuwa na presha na kweli akafanya hivyo, nikaokoa, sikuhama eneo, nikasimama pale pale maana nilijua unaweza kumfuata mpinzani naye ataupiga muda ule ule, na kweli nikaokoa tena," alisema Diarra ambaye alijiunga na Yanga mwaka 2021, akitokea Klabu ya Stade Malien ya jijini Bamako nchini Mali.

Katika tukio hilo, Ateba alitaka kumpiga chenga Diarra, lakini haikufanikiwa, badala yake kipa huyo raia wa Mali, alifanikiwa kuukoa kwa mkono wake wa kulia, aliporuka upande wake wa kulia, ambao ni wa kushoto kwa straika huyo. Kama vile haitoshi mpira aliookoa Diarra ulikwenda kwenye mguu wa kulia wa Joshua Mutale, ambaye alitandika shuti lililombabatiza kipa huyo na kuiokoa Yanga kwenye shambulizi hatari zaidi katika mchezo ambao Simba walilifanya.


Michezo
Jumatano Oktoba 23, 2024
Nipashe

## Neymar arejea uwanjani baada ya mwaka mmoja

UKURASA 22



MSITUNI!...



Beki wa Kati wa Simba, Che Malone Fondoh, akiifungia timu yake bao pekee baada ya kipa wa Tanzania Prisons, Musa Mbisa, kuutema mpira uliopigwa na Kibu Denis, kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya jana. Simba ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# CHE MALONE AITAKATISHA SIMBA MBEYA IKIZOA TATU

●●●Kiwango cha Kibu Denis chazidi kuwatesa mabeki wa timu pinzani baada ya kuonesha...

**Na Faustine Feliciane**

BAO pekee la dakika ya nne ya mchezo lililofungwa na Beki wa Kati, Che Malone Fondoh, jana lilitosha kuipa Simba pointi tatu mbele ya Tanzania Prisons kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Ushindi huo umekuja siku tatu tu baada ya kutoka kupoteza mchezo wa dabi dhidi ya Yanga ambao Simba walikubali kipigo cha bao 1-0.

Katika mchezo wa jana, Che Malone aliifungia Simba bao hilo akitumia makosa ya golikipa wa Tanzania Prisons ambaye mpira uliopigwa na Kibu Denis ulimponyoka na kumpa nafasi mfungaji kuukwamisha nyavuni.

Simba jana walionekana kuutaka ushindi huo kutokana na kucheza kwa nidhamu kubwa kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa mchezo.

Ushindi huo wa jana unaifanya Simba sasa kufikisha pointi 16 baada ya kucheza michezo saba nakupanda mpaka nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

Katika mchezo wa jana, Kocha wa Simba, Fadlu Davids, aliwaanzisha Fabrice Ngoma na Augustine Okajepha wakichukua nafasi ya Abdulrazaq Hamza na Yusuph Kagoma ambao hawakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza baada ya kupata majeraha katika mchezo uliopita dhidi ya Yanga.

Simba jana walifanya mashambulizi kadhaa ambayo hata hivyo hayakuwapa nafasi ya kuongeza idadi ya mabao ambapo katika dakika ya 63 na 53 walikosa

INAENDELEA UK. 23

## Diarra atoa siri kumzuia Ateba

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba moja wa Yanga, Djigui Diarra, amefunguka kwa mara ya kwanza baada ya mchezo wa dabi uliopigwa Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa na kueleza mbinu alizotumia kuokoa hatari kutoka kwa Leonel Ateba, ambayo ingeweza kuipatia Simba bao la kuongoza dakika ya nne tu ya mchezo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, kipa huyo raia wa Mali, alisema pamoja na kucheza michezo kadhaa ya dabi nchini, lakini mechi ya Jumamosi ambayo Yanga ilishinda bao 1-0, ilikuwa ni bora zaidi kuliko zote alizocheza.

"Mechi yangu bora ya Simba na Yanga tangu nifike hapa ni hii ya juzi ya ushindi wa bao 1-0, kwa sababu nilirejea nchini siku ile ile ya mechi, sikuwa fiti sana, nilikuwa na uchovu mkubwa, lakini viongozi wa Yanga, makocha, waliniweka sawa kisaikolojia na kuweza kukaa langoni, ukweli ni mechi bora mno kwangu," alisema kipa huyo.

Diarra alikuwa ametoka kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Mali ambacho kilicheza mchezo wake Oktoba 15, mwaka huu, kikiwa ugenini nchini Guinea Bissau ambapo alikaa langoni na timu hizo kutoka suluhu.

Kabla ya hapo alikaa langoni katika mchezo wa kwanza dhidi ya timu hiyo, Mali ikicheza nyumbani, Oktoba 11 na kushinda bao 1-0, katika mechi za Kundi I, kuwania kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco, kundi hilo likizishirikisha pia nchi za Msumbiji na Eswatini, zamani Swaziland.

Akisimulia jinsi alivyookoa hatari ambayo ilitokea pale straika Mcameroon, Ateba alipokuwa akijaribu kumpiga chenga, alisema siku nyingi alishamsoma mchezaji huyo jinsi anavyocheza, hivyo hakuokoa kwa bahati mbaya.

Alisema yeye ni golikipa, hivyo mbali na mazoezi ya uwanjani, hutenga pia muda wa kuwasoma wapinzani mbalimbali wanaoweza kukutana nao, hasa mastrika jinsi wanavyofunga mabao yao, ili hata ikitokea ajue namna ya kukabiliana nao.

"Huwa naangalia mechi za Simba, nawajua, kwa hiyo nilipoona tumebaki mawili na tayari nimeshamsoma

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >